Nipashe
Jumanne Februari 16, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580493
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**Kampuni** zote mwisho kuagiza sukari nje 2022



UKURASA 2

**Vibali** ajira za wageni kimtandao mwezi ujao

UKURASA 3

UKURASA 11

# Maofisa TBS matatani tuhuma za unyang'anyi

• **Wadaiwa** kudai kwa nguvu mamilioni kiwandani... *Endelea ukurasa wa 3*



Watumishi wa Shirika la Viwango Tanzania, Thomas Mwamlinga (kulia) na Issa Mbaruku wakiwa chini ya ulinzi wa maofisa wa Kikosi cha Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika ofisi za TBS jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutuhumiwa kupokea rushwa ya Sh. milioni 20. **PICHA: JUMANNE JUMA**


## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

**UPEPO WAEZUA NYUMBA, SHULE**

FAMILIA sita katika Kijiji cha Namanguli Kata ya Luchili, wilayani...

**UKURASA WA 5**

**MOHAMED SEIF KHATIB ALILIWA KILA KONA**

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametoa salamu za...

**UKURASA WA 7**

**MASHAHIDI 22 KUJENGA KESI YA KINA MDEE**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayowakabili vigogo 26...


## Kachero asimulia alivyokataa hongo dawa za kulevya

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store




## Askofu KKKT akerwa mauaji wivu kimapenzi

UK. 3

**MICHEZO** **YANGA: KAGERA SUGAR HAWAPONI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza katika ibada ya kumwombea aliyekuwa Mbunge wa Muhambwe, Mhandisi Atashasta Nditiye, Kanisa la Anglikana, Kibondo mkoani Kigoma jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Kachero asimulia alivyokataa rushwa kesi dawa za kulevya

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHAHIDI wa tano wa upande wa mashtaka katika kesi ya ulimaji wa dawa za kulevya aina ya bangi na kufanya mauzo ndani na nje ya nchi, inayomkabili mwekezaji wa kigeni, amedai kuwa mshtakiwa huyo alimwomba wamalizane kimyakimya kwa dau la Sh. milioni 10.

Kesi hiyo inamkabili raia huyo wa kigeni, Damian Jankowski na wenzake watatu, na kuwa mshtakiwa huyo alimwahidi shahidi huku akiahidi kumlipa pesa kila mwezi.

Kesi hiyo namba 79 ya mwaka 2020, inayosikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, Bernazitha Maziku, inawakabili Jankowski raia wa Poland na wastakiwa wenzake Eliwaza Pyuza, Hanif Kanani na Boniface Kessy.

Akiongozwa kutoa ushahidi wake jana mahakamani hapo na Wakili wa Serikali, Verdiana Mlenza, Mkaguzi wa Polisi, Inspekta Hassan Msangi kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), alidai wakati anafanya upekuzi nyumbani kwa Jankowski, mfanyabiashara huyo alimuita pembeni na kumweleza kwamba yuko tayari kumlipa Sh. milioni tano ili aachane naye.

Baada ya kuona ofisa huyo wa polisi hayuko tayari, alipanda dau na kumwambia atampa Sh. milioni 10 na vilevile kila mwisho wa mwezi awe anaenda kwake kuchukua pesa, lakini alikataa na kumwambia binafsi yuko kazini na hawezi kuhitaji hivyo vitu, anaendelea na kazi yake.

Katika hati ya mashtaka, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka manne ambayo ni kulima dawa za kulevya kinyume na kifungu cha 11 (1) (a) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 5 ya Mwaka 2015.

Mshtakiwa wa kwanza, pili na wa tatu wote kwa pamoja wanadaiwa kuwa Februari 8 mwaka jana, huko katika eneo la Njia Panda ya Himo, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, walikutwa wamelima miche ya bangi 729.

Wakati kosa la pili ambalo linawakabili mshtakiwa wa kwanza, pili na wa tatu, ni kusafirisha bangi kinyume na kifungu cha 15A (1) (2) (C) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 15 ya Mwaka 2017 kama ilivyofanyiwa marejeo.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa hao pia wanadaiwa kukutwa na kilogramu 15.6 za bangi katika eneo la Shirimatunda, Manispaa ya Moshi, Februari 8, mwaka jana.

Kosa la tatu ni kusafirisha dawa za kulevya kinyume cha kifungu cha 15A (1) (2) (C) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 5 ya Mwaka 2015 kama ilivyofanyiwa marejeo kifungu cha 9 cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 15 ya Mwaka 2017.

Na kosa la nne ni matumizi ya dawa za kulevya, kinyume na kifungu cha 18 (a) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 5 ya Mwaka 2015.

Mashahidi wengine wa upande wa mashtaka, waliotoa ushahidi wao mahakamani hapo ni pamoja na Mkemia, Joyce Labani na Erasto Lawrence kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na John Msirikali ambaye ni mtunza vielelezo kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini.

Upande wa mashtaka katika kesi hiyo unaongozwa na Wakili wa Serikali, Ignas Mwinuka akisaidiana na Verdiana Mlenza, wakati mshtakiwa wa kwanza, wa pili na watatu katika kesi hiyo, wanatetewa na Wakili FayGrace Sadala. Kesi hiyo itaendelea tena leo.

# Kampuni mwisho kuagiza sukari nje 2022

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imezionya kampuni za kuzalisha sukari nchini kuongeza kasi ya uchakataji wa miwa ya wakulima wa nje, ili kuongeza uzalishaji wa sukari ya kutosha itakayokidhi mahitaji ya ndani kwa kuwa ifikapo mwaka 2022 haitatoa vibali vya kuagiza sukari kutoka nje ya nchi.

Lengo la hatua hiyo ni kukidhi upungufu wa bidhaa hiyo.

Onyo hilo la serikali limetolewa na Waziri wa Kilimo, Prof. Adof Mkenda, alipokuwa akizungumza na uongozi wa mkoa wa Morogoro akiwa ziarani kukagua hali ya uzalishaji sukari na kuzungumza na wakulima wa miwa wa mkoa huo wa ili kubaini changamoto zinazowakabili.

"Mwaka huu vibali vya kuagiza sukari itakayopungua vitatolewa kwa kampuni kwa utaratibu wa kawaida, lakini ifikapo mwaka 2022 hakutakuwa na vibali vya viwanda na ikilazimu basi Bodi ya Sukari ndio itapewa kibali cha kuagiza sukari itakayopungua," alisisitiza Prof. Mkenda.

Waziri Prof. Mkenda alisema serikali inafuatilia kwa karibu utendaji kazi wa viwanda vya kuchakata sukari nchini kuona kama vinaweka mikakati ya kuongeza uzalishaji wa sukari kwa kushirikiana na wakulima wa miwa kwa kuwa mpango wa serikali ifikapo mwaka 2022 kuacha kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje na badala yake izalishwe hapa hapa kwa kutumia viwanda vilivyopo.

"Tatizo letu la upungufu wa sukari halitokani na kukosa miwa bali ni uwezo mdogo wa viwanda kuchakata miwa yote ya wakulima nchini hali inayosababisha baadhi ya miwa ya wakulima kukosa soko," alisema Waziri Mkenda.

Alisema Wizara ya Kilimo ina mkakati wa kuhakikisha miwa yote ya wakulima inachakatwa na viwanda vilivyopo ili kuondoa tatizo la upungufu wa sukari na kuwa utaratibu wa sasa viwanda kupewa vibali vya kuagiza sukari nje hauna manufaa kwa taifa.

Waziri Mkenda alisema Ili kuwa na uhakika wa sukari, wizara inahamasisha matumizi ya mbegu bora na kilimo cha umwagiliaji pamoja na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vipya vya sukari.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emanuel Kalobelo, alisema mkoa huo una viwanda vitatu vya kuzalisha sukari ambavyo bado uzalishaji wake ni mdogo hali inayopelekea miwa ya wakulima kukosa soko na kuharibika.

Alivitaja viwanda hivyo na uzalishaji wake ni Kilombero Sugar Ltd na Kilombero Sugar II kwa pamoja huzalisha (tani 126,000) na kiwanda cha Mtibwa (tani 50,000), huku uzalishaji wa miwa kwenye bonde la Kilombero unaofanywa na wakulima wadogo umefikia wastani wa tani 800,000 hadi 1,000,000 na uwezo wa kiwanda cha Kilombero ni kuchakata tani 600,000 tu za wakulima wadogo kwa mwaka.

"Mfano uzalishaji wa miwa ya wakulima wadogo outgrowers ni kati ya tani 800,000 hadi 1,000 000 na uwezo wa kiwanda ni tani 600,000," alisema Kalobelo.

Kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Sukari Tanzania, uzalishaji kwa mwaka ni takribani tani 300,000 ambapo kwa mwaka 2020/21 ulifikia tani 377,527 na mahitaji ya sukari kwa matumizi ya kawaida na viwandani ni tani 655,000

Viwanda vinavyozalisha sukari ni Kilombero, Mtibwa, Kagera, TPC na Manyara.

**HABARI KITAIFA**

## Askofu KKKT akerwa mauaji wivu kimapenzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria mikoa ya Shinyanga na Simiyu, Dk. Emmanuel Makala, ameeleza kukerwa na mauaji ya wivu wa kimapenzi ambayo yanaendelea katika Mkoa wa Shinyanga.

Makala alibainisha hayo juzi kwenye hafla ya kusimikwa msaidizi wake, Yohana Nzelu, na pia kusimikwa mashemasi kuwa wachungaji rasmi, pamoja na wajumbe wa Halmashauri Kuu wa Dayosisi wa Kanisa hilo.

Alisema Mkoa wa Shinyanga umekithiri kwa matukio ya mauaji yatokanayo na wivu wa kimapenzi, na kuwataka wanandoa kama wana migogoro ya kifamilia watafute suluhu na siyo kujichukulia sheria mkononi, na hatimaye kupigana na kusababisha mauaji.

"Mauaji haya ya wivu wa kimapenzi baadhi yake pia hutekelezwa na watu wageni ambao hukodiwa kufanya mauaji, hivyo kuna haja ya serikali kuwasaka wageni ambao hawajulikani, kuanzia ngazi ya mtaa, kitongoji na kijiji, na kisha kuwafukuza," alisema Askofu Makala.

Pia alisema viongozi wa dini wanaishukuru serikali kwa kuendelea kutoa uhuru wa kuabudu, licha ya kupitia kipindi hiki kigumu cha janga la corona, pamoja na kushirikiana nao kuhakikisha amani ya nchi inazidi kutawala.

Kwa upande wake mgeni rasmi Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabaganga Talaba, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, aliwataka viongozi wa dini kuendelea kukemea maovu ndani ya jamii, ili watu waishi kwa upendo na amani.



Mkuu wa Wilaya ya Urambo, mkoani Tabora, Angelina Kwingwa, akipewa maelezo na mwandishi wa habari mwandamizi wa gazeti la Nipashe Salome Kitomari, alipotembelea ofisi za gazeti hili Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maofisa wa TBS matatani

**Na Joseph Mwendapole**

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, ameliagiza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuwasimamisha kazi maofisa wake watatu kwa tuhuma za kufanya unyang'anyi katika Kiwanda cha Smart kilichopo Kijitonyama, jijini Dar es Salaam wakitaka kulipwa Sh. milioni 100 kwa nguvu.

Aidha, ameagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kushirikiana na Polisi kufanya uchunguzi dhidi ya maofisa hao ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Naibu Waziri Kigahe alitoa maelekezo hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya TBS, jijini Dar es Salaam jana.

Aliwataja maofisa hao kuwa ni Ofisa Viwango wa TBS, Sulemain Banza, Ofisa Usafirishaji, Thomas Elisha na dereva, Issa Dodo pamoja na watu wengi ambao hakuwataja majina waliojitambulisha kuwa polisi.

Alisema Februari 12, mwaka huu, watu hao walienda kwenye kiwanda hicho wakitaka kufanya ukaguzi kwa madai kuwa kinazalisha bidhaa kwa kutumia malighafi zilizoisha muda wake.

Alisema maofisa hao hawakuwa wametumwa na shirika hilo na kwamba Banza aliingilia majukumu ya watu wengine kwenda kufanya ukaguzi, wakati kazi zake ni ofisa viwango na sio mkaguzi. Kwa mujibu wa Naibu Waziri Kigahe, baada ya kufika kiwandani hapo walitaka walipwe Sh. milioni 100 ili waweze kuachana na suala hilo, lakini mwenye kiwanda hakuwa na kiasi hicho cha fedha.

Alisema baada ya hapo walitaka walipwe Sh. milioni 50, ambazo nazo mwenye kiwanda hakuwa nazo ndipo walipotaka Sh. milioni 20, ambapo mmiliki wa kiwanda hicho kwenye akaunti yake alikuwa na Sh. milioni 10 na mkewe Sh. milioni 10.

Alisema mmiliki wa kiwanda hicho, mke wake na mhasibu walisindikizwa wakiwa chini ya ulinzi wa watu waliojitambulisha kuwa ni polisi, huku wakiwa wamenyang'anywa simu zao hadi benki na walipotoa fedha Sh. milioni 20 na kuwakabidhi kisha kuwaachia.

Alisema baada ya kuachiwa ndipo mwenye kiwanda na mkewe walipiga simu wizarani na kutoa taarifa za tukio hilo.

Naibu Waziri Kigahe alisema kitendo hicho ni unyang'anyi wa hali ya juu na hakikubaliki katika kipindi hiki ambacho serikali imetengeneza mazingira kuvutia wawekezaji kujenga viwanda.

"Matukio haya kwa wawekezaji hayawezi kufumbiwa macho na tunalaani tukio hili," alisema na kusisitiza kwamba wahusika wa tukio hilo wametumia utashi wao kufanya unyang'anyi, hivyo serikali haiwezi kuwavumilia hata kidogo.

Hivyo, mbali ya kuitaka TBS kuwasimamisha kazi ameitaka ichukue hatua nyingine za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za kazi.

Aidha, alitoa wito kwa watumishi wote wa taasisi zilizo chini ya wizara hiyo, kuzingatia maadili ya kazi na serikali haitasita kuchukua hatua kali kwa watakaobanika kujihusisha na vitendo hivyo.

# Vibali ajira za wageni kimtandao mwezi ujao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa utoaji vibali vya ajira kwa wageni ifikapo Machi 20, mwaka huu, ili kuondoa mianya ya rushwa, vishoka na kurahisisha upatikanaji wake.

Aidha, imesema ofisa kazi yeyote wa mkoa atakayeshindwa kutatua vikwazo kwa wawekezaji na kusubiri viibuliwe kwenye ziara za viongozi wa kitaifa atawajibishwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alitoa maagizo hayo jana, alipokuwa akifungua mafunzo ya awamu ya kwanza kwa maofisa 20 ambayo yamefadhiliwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO).

"Tunaenda kuweka mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa vibali vya ajira za wageni, kila kitu kimekamilika, majaribio ya mfumo yamefanyika na mfumo huu usomeke na mifumo mingine iliyopo nchini... Kabla ya Machi 20, mwaka huu, uwe umezinduliwa," alisema.

Alisema mfumo utaondoa vitendo vya rushwa na vishoka na kwamba kuna maofisa kazi kwa kuwa mawakala wamekamatwa kwa kupokea rushwa na kutoa vibali feki.

"Sasa tunakwenda kwenye mfumo huko ndio tutaonana vizuri, wale waliokuwa na tabia kwenye mfumo huu waache wapo wachache tunawajua na baadhi yao tumechukua hatua," alisema.

Alibainisha faida za mfumo huo kuwa utasaidia kuwa na takwimu za wageni walioajiriwa na ujuzi wao, kutochelewesha vibali na lini utafanyika urithishaji wa ujuzi.

"Mfumo utasaidia kutambua ni maeneo gani labda ujuzi kwetu uhaba ndani ya taifa, nimeulilia huu mfumo kwa miaka minne sasa umefika mahali pazuri," alisema.

Mhagama alisema tathmini ya Sheria ya Utoaji Vibali kwa wageni ifanyike ili kukidhi mahitaji ya sasa.

Kuhusu uzembe wa maofisa hao, Waziri Mhagama alisema kumekuwapo na uzembe wa kushindwa kushughulikia malalamiko ya wawekezaji na kuyaacha yaibuke kwenye ziara za viongozi.

"Inanisikitisha inavyotokea viongozi wa kubwa wa serikali wa ngazi ya Taifa, inafika mahali wawekezaji wafanyakazi wanalalamika kwao wakati nyie mpo, hili ni jambo la kushangaza juzi pale kwa Rais(John Magufuli) Morogoro, mwekezaji alikuwa akilalamika hajapewa vibali vya ajira vya watumishi anaohitaji kwenye kiwanda chake," alisema.

Aliwataka kujua maeneo yote ya uwekezaji yanayoanzishwa kwenye maeneo yao ili kujua uhitaji kero zao na kuzishughulikia.

"Itakapotokea tena kiongozi yeyote amefika kwenye mkoa wowote kufungua eneo la uwekezaji, kiwanda halafu wawekezaji wakalalamika kuhusu utekelezaji wa matakwa ya uwekezaji wao ya sheria za kazi ni tatizo, atakayewajibika ni ofisa kazi wa eneo husika, haipendezi kusubiri viongozi wakuu wawe watatuzi wa migogoro," alisema.

Aliwaagiza kusimamia mikataba ya ajira husuan ya madereva na kwamba ofisi yake ilishakutana na wadau na kutengeneza mpango kazi.

"Eneo hili bado lina matatizo mengi, jambo hili haliwaachi nje ya majukumu yenu, jambo hili linataka ushirikishwaji wa madereva na waajiri, kabla ya Machi au Aprili jambo hili likamilike," alisema.

# Wilaya kujenga shule maalum ya wasichana

**Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro imeamua kujenga shule mpya nne za sekondari ikiwamo moja maalumu kwa wanafunzi wa kike, ili kuondokana na changamoto za ukosefu wa vyumba vya madarasa kila mwaka kwa wanafunzi.

Katika hatua ya awali imetenga Sh. milioni 400 kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambazo zimeanza kutumika kwenye uboreshaji elimu ya sekondari na ujenzi wa shule mpya kwa mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Asajile Mwambambale, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati ya maboresho kwenye sekta ya elimu ya msingi na sekondari wilayani humo.

Mwambambale alisema ujenzi wa shule ya sekondari maalumu ya wanafunzi wa kike inayojengwa eneo la Manzese, Kilosa Mjini upo katika hatua ya kati baada ya kumalizika kwa msingi wake.

"Tupo katika maandalizi makubwa ya kuona wanafunzi wanaofaulu darasa la saba wote wanaingia kuendelea na masomo ya sekondari bila kuachwa, na kwa sasa waliofaulu kuingia kidato cha kwanza wapo madarasani," alisema Mwambambale.

Alisema kwa sasa wanakamilisha ujenzi wa madarasa mawili kwenye Shule ya Sekondari Magole na darasa moja katika Shule ya Sekondari Mikumi.

Alisema ili kuondokana na uhaba wa vyumba vya madarasa kila mwaka, wilaya imeamua kujenga shule moja maalumu ya sekondari ya wasichana eneo la Manzese mjini Kilosa.

" Ujenzi wa shule hii kwa sasa upo katika hatua nzuri na hadi mwisho wa mwaka huu, itakuwa imekamilika na mwaka ujao wa masomo (2022) itakuwa tayari kuchukua wanafunzi wa kike wa Wilaya ya Kilosa," alisema Mwambambale.

Alisema wilaya hiyo pia imekusudia kujenga shule nyingine tatu katika eneo la Mikumi ili kukabiliana na idadi kubwa ya wanafunzi wanaofaulu shule za msingi zilizopo kwenye Tarafa ya Mikumi.

" Ujenzi wa shule hizi unatarajia kuanza mwezi Machi, mwaka huu na hadi kufikia mwezi Desemba zitakuwa zimekamilika ili lengo ni wanafunzi wapya watakapochaguliwa mwaka 2022 wawe wanapata masomo yao moja kwa moja," alisema Mwambambale.

# Upepo waezua nyumba za familia, majengo ya shule

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

FAMILIA sita katika Kijiji cha Namanguli Kata ya Luchili, wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma, zimekosa makazi baada nyumba zao kuezuliwa na upepo mkali.

Upepo huo ulioambatana na mvua kubwa mwishoni mwa wiki na kuziacha familia hizo zikihangaika kwa kukosa makazi.

Tukio hilo limetokea majira ya jioni, ambapo mvua iliyoambatana na upepo uliezua nyumba tano za familia moja na moja ya familia nyingine ya karibu.

Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Namanguli, Hija Siwea, alisema katika tukio hilo hakuna watu walioathirika kwa kuwa wakati wa matukio hayo ya kuezuliwa nyumba hizo yanatokea familia za nyumba hizo zilikuwa hazijarudi kutoka mashambani.

Siwea alisema uongozi wa kijiji kwa kushirikiana na Diwani wa Kata ya Luchili, Othmani Njovu, waliwatembelea wananchi waliopatwa na tatizo hilo kwa lengo la kutoa pole kwa waathirika.

Upepo huo pia uliezua Shule ya Msingi Kilangalanga katika Kata ya Luchil, madarasa mawili ya Shule ya Msingi Ligunga katika Maamlaka ya Mji Mdogo wa Lusewa darasa moja pamoja na Shule ya Msingi Msisima darasa moja katika mamlaka.

Mkurugenzi wa Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Evance Nachimbinya, alitembelea shule zilizopatwa na majanga hayo na kuchukua hatua ya kuezeka majengo yote yaliyoezuliwa na upepo huo kwa lengo la kuhakikisha shule zote zinaendelea na masomo kama kawaida.

Mvua zinazoendelea kunyesha wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma zimekuwa zikiambatana na upepo mkali na radi.




Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya CCECC wakijenga ukuta katika eneo la Ubungo stendi ya mkoa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Dereva matatani tuhuma za kusafirisha wahamiaji haramu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani, limemkamata dereva wa gari lenye namba za usajili T 703 DTR aina ya Hiace, mkazi wa Uyole Mbeya akituhumiwa kisafirisha wahamiaji haramu sita raia wa Malawi. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema dereva huyo ambaye jina linahifadhiwa alikamatwa juzi katika eneo la Tanita Wilaya ya Kibaha majira ya saa nne asubuhi akitokea Mbeya kwenda jijini Dar es Salam. Wankyo alisema katika mahojiano ya awali raia hao wa kigeni wanadaiwa kuelekea jijini Dar es Salaam kwa ajili ya biashara za kuuza baa na kusuka.

Katika tukio lingine Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani linamshikilia Mhina Mrisho (42), mkazi wa Miono Wilaya ya Bagamoyo, kwa tuhuma za kumjeruhi kwa risasi Tatu Bakari (55), mkazi wa Miono.

Kamanda Wankyo alisema tukio hilo lilitokea Februari juzi, asubuhi, ambapo Tatu alijeruhiwa kwa kupigwa na risasi katika mguu wake wa kulia na mtuhumiwa Mhina akiwa shambani kwake.

Wankyo alisema baada ya mtuhumiwa kukamatwa alipopekuliwa alikutwa akiwa na bunduki mbili aina ya gobore, ambazo anamiliki kinyume cha sheria.

Kamanda Wankyo ametoa rai kwa watu wanaomiliki silaha pasipokuwa na vibali kuzisalimisha kwenye vituo vya polisi kwa hiari ndani ya siku saba kabla hawajakamatwa. Aidha, alitoa wito kwa madereva na wananchi wenye tabia ya kusafirisha wahamiaji haramu kuacha biashara hiyo, badala yake watafute kazi nyingine.

HABARI KITAIFA

## Waziri Mkuu ataka Nditiye akumbukwe kwa vitendo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kaasim Majaliwa, amesema sifa na maneno mazuri ambayo yamesemwa kuhusu aliyekuwa Mbunge wa Muhambwe, Mhandisi Atashasta Nditiye, yatakuwa na maana tu endapo matendo mema aliyoyatenda wakati wa uhai wake yataenziwa na kuendelezwa.

Akizungumza katika ibada ya kumwombea marehemu, katika Kanisa la Anglikana la Kibondo, mkoani Kigoma, Waziri Mkuu amesema serikali inathamini mchango alioutoa wakati wa uhai wake na ndiyo maana Rais Magufuli amemtuma amwakilishe katika msiba huu.

Amewataka wana-Muhambwe, wabunge na Watanzania kwa ujumla wamwombee marehemu ili Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. "Nawasihi tuwe karibu na familia ya marehemu kama tulivyokuwa wakati wa uhai wake, hatua ambayo naamini itawapa faraja wanafamilia."

Naye Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson alisema Spika Ndugai amepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Nditiye kwani alikuwa na mchango mkubwa katika Bunge kutokana na michango yake mizuri ya uzalendo, mapenzi makubwa kwa wapigakura wake na Taifa pia.

"Kwa mara ya mwisho, Mhandisi Nditiye alichangia katika Bunge lililopita tarehe 9 Februari, 2021 wakati nikiwa kwenye kiti na hakuna aliyedhani kuwa leo tusingekuwa naye. Niwasihi ndugu zangu tuwe tayari wakati wote kwani hakuna ajuaye siku yake ya mwisho," alisema.

Mwakilishi wa Wabunge wa Mkoa wa Kigoma ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema anaishukuru serikali hasa Rais, Dkt. John Magufuli, Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa misaada waliyoitoa wakati wa kumuuguza, wakati wa msiba na katika mazishi.

Aliishukuru pia Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Spika Job Ndugai, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai na wabunge wote kwa ushiriki wao wa hali na mali katika ugonjwa, msiba na mazishi ya Mhandisi Nditiye.

Akitoa salamu zake, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, alisema Mhandisi Nditiye alitumia muda wake mwingi kukutana na viongozi wa mkoa huo ili kujadili na kushauriana masuala mbalimbali yaliyohusu maendeleo ya mkoa huo.

Viongozi wengine walioshiriki mazishi hayo ni Mhandisi Isaack Kamwelwe, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante ole Gabriel, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel na baadhi ya wabunge.

Mhandisi Nditiye alizaliwa 17, Oktoba 1969, Wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma. Alisoma shule ya msingi Kabwigwa kuanzia mwaka 1975 hadi 1981 na baadaye alijiunga na Chuo cha Ufundi Dar es Salaam ambako alisoma kuanzia mwaka 1984 hadi 1986 na kutunukiwa cheti cha uhandisi.

Katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano, Mhandisi Nditiye alikuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anayeshughulikia Mawasiliano.

Taarifa ya kifo chake ilitolewa bungeni Februari 12, 2021 na Spika wa Bunge, Job Ndugai ambaye alisema kuwa kifo hicho kimetokana na ajali aliyoipata Jumatano, Februari 10, 2021 katika eneo la Nanenane, jijini Dodoma.

# Mohamed Seif Khatib aliliwa kila kona

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametoa salamu za rambirambi kufuatia kifo cha Dk. Mohamed Seif Khatib na kusema taifa limempoteza kiongozi hodari, shupavu alipenda kufanya kazi kwa maslahi ya taifa na muungano.

Katika salamu zake kwa ndugu wa familia, Dk. Mwinyi alisema amepokea kwa mshtuko mkubwa taarifa za kifo cha Khatib ambaye anamkumbuka kuwa kiongozi mahiri katika Jamhuri ya Muungano kwa kushika nafasi mbalimbali za uwaziri.

"Nimepokea taarifa ya kifo cha marehemu Dk. Mohamed Seif Khatib kwa mshtuko mkubwa na simanzi...namfahamu sana marehemu ambaye alifanya kazi kwa muda mrefu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa waziri," alisema.

Aidha alisema kwa upande wa Zanzibar Dk. Khatib ni Mwenyekiti wa Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) pamoja na mjumbe wa kamisheni ya utumishi serikalini.

Khatib alifariki dunia mapema asubuhi jana katika Hospitali ya Al-Rahma iliyopo Kilimani mjini Unguja na anatarajiwa kuzikwa leo kijijini kwao Umbuji Wilaya ya Kati Unguja.

Mapema wanasiasa wakongwe waliopata kuwa mawaziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano na makatibu wakuu wa umoja wa vijana wa (UVCCM) pamoja na wabunge wastaafu wamekielezea kifo cha kada wa CCM kuwa pigo katika chama, huku mchango wake hautosahaulika katika kuwaendeleza na kuwaibuwa wanasiasa vijana na umoja wake kuwa imara na tegemeo la ushindi wa CCM.

Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mbunge mstaafu wa Jimbo la Donge, Ali Ameir Mohamed, alisema kifo cha Khatib (70), ambaye alikuwa naye pamoja katika Baraza la Mawaziri la Muungano na Mzee Benjamin Mkapa kimeacha pigo kubwa.

Alisema Khatib alikuwa kiongozi aliyekomaa na kulelewa katika misingi ya uadilifu, uhodari na kuchapa kazi huku akiwa na mapenzi makubwa ya chama na jumuiya za chama ikiwamo Umoja wa Vijana wa UVCCM.

"Khatib alikuwa miongoni mwa makada wa Chama Cha Mapinduzi aliyelelewa katika msingi ya kimapinduzi ya kufanya kazi, uadilifu na kupenda jumuiya za chama ikiwamo UVCCM," alisema.

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa UVCCM, Sukwa Said Sukwa, alimwelezea marehemu Khatib kuwa kada aliyekulia umoja wa huo na kuutumikia kwa nguvu zake katika ngazi mbalimbali kuanzia katibu mkuu hadi mwenyekiti wa umoja huo taifa.

"Huyu alikuwa mwalimu wetu katika fani mbalimbali kuanzia darasani hadi katika siasa za ukombozi na kupigania uhuru wa nchi yetu na mapinduzi," alisema Sukwa.

Aliyekuwa Mbunge wa Kikwajuni, Parmukh Hoogan Sikh, alisema marehemu alikuwa mshauri huku akiwaelekeza wabunge wapya nini cha kufanya katika kuwatumikia wananchi ikiwamo wapigakura na kujenga hoja ndani ya Bunge.

"Nilikuwa naye katika bunge kipindi cha miaka kumi...tulikuwa tukiomba ushauri wa aina mbalimbali ambapo katika jimbo langu la Kikwajuni ndipo marehemu alipoanzia katika safari ya kisiasa," alisema.

Khatib alizaliwa Januari 10, mwaka 1951, katika kijiji cha Umbuji wilaya ya kati na kupata elimu yake katika Shule ya Uzini kwao Umbuji katika miaka ya 1968 na baadaye kusomesha katika Chuo cha Ualimu cha Nkruham mjini Unguja katika miaka ya 1970.

Khatib alijitosa katika siasa na kujiunga na UVCCM na kufanikiwa kushika wadhifa wa mwenyekiti wa umoja huo taifa katika mwaka 1978 hadi 1982 na baadaye kushika wadhifa wa katibu mkuu katika mwaka 1982 hadi 1988.

Alijitosa kuwania ubunge Jimbo la Uzini katika mwaka 1995 kwa muda wa vipindi vitatu na kufanikiwa kushika nafasi mbali mbali za uwaziri ikiwamo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) katika mwaka 2008 pamoja na Waziri wa Nchi anayeshughulikia habari kuanzia Januari 4 katika mwaka 2006.

Hatua hiyo ilimwezesha marehemu kufanya katika utumishi wa marais watatu wa Muungano akiwamo Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, Hayati Rais mstaafu Benjamin Mkapa na Rais mstaafu Jakaya Kikwete.

Katika enzi za ujana wake aliwahi kuwa mchezaji mahiri wa mchezo wa mpira wa miguu na kuzichezea timu maarufu za mjini ikiwamo Kikwajuni, huku akiwa mahiri zaidi katika utunzi wa mashairi na uandishi wa vitabu pamoja na nyimbo za taarab akiwa mwimbaji katika jukwaa.

Marehemu alitunukiwa shahada ya Uzamivu katika Chuo Kikuu cha Dodoma tarehe 25, mwaka 2011 na Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano Benjamin Mkapa.

Ni shahada ya kwanza ya juu ya uzamivu kutolewa katika Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo marehemu alitunukiwa kwa unyenyekevu mkubwa.


Alipata shahada ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam katika mwaka 1978 na shahada ya pili alipata katika mwaka 1982 Uingereza.

Khatib amekuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi kwa muda mrefu pamoja na Kamati Kuu ya CCM ambapo aliingia kupitia UVCCM na kufanikiwa kuongoza bodi mbalimbali ikiwamo za magazeti ya Uhuru na Mzalendo kwa nyakati tofauti.

Hadi kifo chake Khatib pia ni mmiliki wa kampuni za vyombo vya habari za Zenji Media ikiwamo magazeti, redio na televisheni akiwa mwanzilishi wa kwanza wa vyombo vya habari binafsi Zanzibar baada ya kufunguliwa kwa milango ya uhuru wa vyombo vya habari na uwekezaji wake.

Akiwa Waziri wa Habari na Utamaduni, Khatib ndiye mwanzilishi wa gazeti la Kiswahili la serikali ya HABARILEO ambalo lilianzishwa kwa ajili ya kutoa fursa kwa wasomaji kupata taarifa sahihi za serikali katika kipindi cha Rais mstaafu Jakaya Kikwete.

Hadi anakumbukwa na mauti kwa mujibu wa watu na marafiki zake alikuwa katika harakati za kutayarisha kitabu cha maisha yake ambapo alihamasika kufanya hivyo baada ya Rais mstaafu Benjamin Mkapa kutunga kitabu kinachoelezea maisha yake.



Marehemu Dk. Mohamed Seif Khatib

# Anayedaiwa kuuawa na kaka azikwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWILI wa marehemu Magreth Mushi (50), mkazi wa Kijiji cha Urauri, Kata ya Reha wilayani Rombo, anayedaiwa kuuawa na kaka yake, ulizikwa jana katika makaburi ya familia katika kijiji cha Singa Kati, wilayani Moshi mkoani Killimanjaro.

Anadaiwa kuuawa na kaka yake, Leoni Mushi (39), kwa kumkata na mapanga kichwani baada ya mzozo kati yao kuhusu mauzo ya nyanya.

Akizungumza jana wakati wa maziko, mtoto wa marehemu, Francis Kisoka, alisema: "Jambo hili limenisikitisha sana, naiomba serikali kuingilia kati katika kupata haki ya mama yangu, pamoja na kuimarisha ulinzi katika kitongoji hicho kwani mtu huyu amekuwa tishio kwa familia."

Akizungumza katika ibada fupi ya maziko katekista, Patrick Chuwa, aliitaka jamii kuacha matukio ya kihalifu. "Hili tukio linasikitisha sana, naomba serikali kuangali matukio kama haya, na watu mnapotishiwa toeni taarifa maeneo husika, Jeshi la Polisi angalieni kwa umakini hasa kuna watu wanaokuja kutoa taarifa za vitisho," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sheria ilinde wanawake kudhalilishwa

**MWISHONI** mwa wiki, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, katika semina ya wabunge wanawake alionyesha kukerwa na tabia ya watu kuwatuhumu viongozi kuwa wamekuwa wakitoa nafasi za uongozi kwa wanawake kwa upendeleo kutokana na uhusiano walionao.

Aidha, alishauri kutungwa kwa sheria kali dhidi ya udhalilishaji wa wanawake, kwa kuwa tabia hiyo haipaswi kufumbiwa macho kwa sababu kwenye jamii baadhi ya watu wapo wanaoamini mwanamke hawezi kupata nafasi kwa haki bila kupendelewa kwa sababu ya uhusiano na mtu.

Alisema wanawake hawapaswi kuendelea kuvumilia kashfa hizo zenye kuwadhalilisha, na anapaswa kuwa na misimamo mikali dhidi ya vitendo hivyo.

Kero hii ni ya muda mrefu ambayo ilianza enzi na enzi kwa lengo la kudunisha jinsia moja na kuipa nyingine nguvu, ili kuendelea kuitawala na hii ilifanyika na kuwekewa misingi kwenye taratibu, kanuni, sheria na katiba ya nchi.

Mathalani, Sheria ya Ndoa inataja umri wa mwanamke kuolewa ni kuanzia miaka 13, lakini Katiba inasema mtoto ni chini ya miaka 18, pia Sheria ya Ardhi haikutoa nafasi kwa mwanamke kumiliki ardhi jambo ambalo lilisababisha wengi kukosa haki zao, lakini baadaye yalifanyika mabadiliko na sasa ana haki ya kumiliki.

Pia iliruhusu wanandoa kumiliki ardhi na mali kwa pamoja, tofauti na zamani mali zote zilikuwa za mwanaume na siku akifa basi mwanamke hana haki.

Nyingine ni haki ya elimu ilipewa nafasi kwa mtoto wa kiume, huku wakike akiambiwa asubiri kuolewa, na pia ukeketaji na ndoa za utotoni ni moja ya mambo yaliyofanyika kunufaisha jinsia moja.

Katika hali ya kutaka kutawala jinsia nyingine wanawake waliojitokeza kuwania nafasi hususani za kisiasa walipachikwa majina mabaya kiasi cha wengine kuachwa na waume zao kwa madai kuwa wakiwa na uwezo wa kifedha au madaraka basi hawatastahili kuwa mke wa mtu.

Matukio haya hushamiri zaidi wakati wa kampeni za majukwaani na hasa katika ulimwengu wa digitali ambao mtu mwenye kifurushi cha intaneti na simu ya kisasa basi anaweza kutuma ujumbe wowote kwenye mitandao ya kijamii kwa lengo la kumiza jinsia fulani.


Alichokisema ni tatizo kubwa na ndiyo maana wanaharakati mbalimbali wamefanya mikutano, uragibishi na semina kwa wanawake ili kuwaandaa kushika nafasi hizo, ili kuongeza idadi ya wanawake katika nafasi za maamuzi ambayo wanapungua kila siku kutokana na mifumo ya malezi na mingineyo.

Kwa sasa watu wanatumia majina feki kutukana watu hasa wale waliojitokeza kuwania nafasi za kisiasa, hii inapunguza idadi ya wanawake katika majimbo na kata, huku wakisubiri viti maalum ambavyo wakati mwingine wanauwezo wa kuongoza jimbo.

Tunapongeza maono ya kiongozi huyu kuishauri serikali kutunga sheria kali dhidi ya udhalilishaji wa wanawake.

Hili litafanikiwa zaidi ikiwa msisitizo utaanza ndani ya vyama kuona kwamba wanawake wanaweza kugombea kwenye majimbo na kata, ikiwa ni pamoja na nafasi za urais na makamu wa rais.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Vianze viwanda viuatilifu asilia

Na Mwandishi Wetu

**KUNA** kilio cha ongezeko la maradhi kama saratani na changamoto lukuki kiafya zinahusishwa na matumizi ya kemikali za sumu kwenye kilimo na ufugaji. Leo kuna dawa za kila aina kutibu mifugo, mazao na za kuhifadhi vyakula hasa nafaka na mazao ya mikunde ambazo huenda si salama.

Ndiyo maana kuna haja sasa kwa serikali na wadau kusisitiza ugunduzi na matumizi ya kemikali za asili kudhibiti magonjwa ya mimea na ikiwezekana kujenga viwanda na kuzizalisha kwa wingi. Kutumia viuatilifu vya viwandani ni jambo linaloongeza hasara kuliko tija hivyo ni bora serikali na wadau washirikiane kufanikisha utafiti wa upatikanaji wa dawa pamoja na mbolea za asili ambazo hazitokani na kemikali za viwandani.

Ni wazi kuwa dawa mbalimbali ambazo hutumika kwenye kuzalisha mazao kuanzia sumu za kunyunyuzia magugu, 'booster' za kuinua afya za mimea na mbolea ambazo hutumiwa kupandia na kukuzia na mwisho kuyahifadhi kwenye vihenge. Yote hayo ni hatari na huenda ndicho chanzo cha magonjwa hasa yanayohusiana na saratani na uvimbe mwilini.

Kuna wakulima wanaotumia dawa za asili kama za mwarobaini na alovera kuna haja ya serikali na watafiti wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kuzifanyia uchunguzi ili kufahamu sumu zake na kiwango kilichomo na uwezo wa kemikali hizo kuua au kudhibiti wadudu katika mimea na kama kuna athari kwa wanadamu pia.

Pamoja na kujua hali hiyo na pia kutambua athari zake kwa afya na mazingira ili kujua iwapo kuna tija ama hasara kiafya kwa mlaji na mazingira yake. Zipo taarifa kuwa mwarobaini, umeshafanyiwa utafiti na kugundulika kuwa unaweza kudhibiti baadhi ya wadudu kwenye

mimea ni vyema dawa hizo zikaendelea kutafitiwa na kutumiwa na wakulima kote nchini kukabiliana na magonjwa na wadudu waharibifu na serikali kujitahidi kujenga viwanda vya viuatilifu vya asili ili kukabiliana na athari za kemikali.

Wakati taasisi kama ile ya Utafiti wa Dawa za Binadamu (NIMR) ikielekeza nguvu kwenye tiba asilia ni vyema pia kuangalia namna ya kuisaidia SUA kufanya utafiti na majaribio pamoja na kutoa matokeo ya utafiti wa dawa hizo zisizo na kemikali kwa wakulima ili wanufaike na kilimo hai (organic farming) kinachookoa maisha na mazingira.

Ukiangalia mifano mingi kuna dawa aina mbalimbali na kundi la kwanza ni zile ambazo zinapoingia ardhini au kwenye maji zinadumu mathalani, DDT iliyotumika miaka ya nyuma na kuonyesha athari kubwa. Zipo dawa za kahawa kama 'samathayon', za bungua kama 'parathayon' na nyingine nyingi ambazo zinadaiwa kuwa zimesababisha watu wengi kuathirika.

Mbali na binadamu zimewaathiri wanyama na mimea pia. Kuna maelezo ya kitaalamu kuwa watu wanapokula dawa kama hizi sumu yake inajikusanya kwenye seli za mafuta na kuleta madhara yanayosababisha kifo.

Zipo ambazo zinaondoka haraka kwenye mazingira, lakini matumizi yake hayafanyiki kwa usahihi kutokana na kupuliziwa kwenye mmea muda mfupi na mazao kupelekwa sokoni yakiwa

na sumu na watu kuendelea kula bila kufahamu. Yote hayo yanahamasisha kuwa na viwanda vya kutengeneza kemikali za asili ili kuokoa maisha. Ikumbukwe mazingira yasipokuwa salama afya haziwezi kuwa kamilifu hivyo ni wakati wa kuzalisha vyakula vinavyowaacha watu katika hali bora bila kuathirika.

Pamoja na sumu zinazonyunyizwa kwenye mimea kuna mbolea zinazowekewa

ama kuikuza au kuipandia nazo zina kemikali ambazo, wakati mwingine huendelea kuleta athari kwa watumiaji na mazingira.

Wapo wakulima ambao humwagilia mbolea ya chumvichumvi kwenye mazao na kuyauza muda mfupi baadaye, jambo linalosababisha wateja kula mbolea hiyo ambayo haijachakatwa na kufyonzwa na mmea hali inayotishia afya ya walaji.

HABARI KITAIFA

# Madiwani wacharuka matokeo mabaya la 7

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Songea limesikitishwa na wasimamizi wa Idara ya Elimu kushindwa kusimamia taaluma na kusababisha halmashauri hiyo kushika mkia kati ya nane za Mkoa wa Ruvuma kwenye matokeo ya darasa la saba 2020.

Matokeo ya Mtihani wa Taifa wa darasa la saba 2020, yanaonyesha kuwa halmashauri hiyo ilifaulisha kwa asilimia 66.66, hivyo kuwa ya mwisho kimkoa.

Akizungumza kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Menas Komba, ameiagiza Idara ya Elimu Msingi na Sekondari kuanza kuchukua hatua kwa wasimamizi na walimu ambao hawafanyi kazi.

"Sisi kama Baraza la Madiwani sasa tutashughulika nao, tunataka Halmashauri ya Songea kielimu tuwe juu, serikali imetoa fedha za utoaji wa elimu bure, waratibu elimu kata wamepewa pikipiki, wanalipwa posho za madaraka shilingi 250,000 kila mwezi, wakuu wa shule za msingi wote wanalipwa posho za madaraka, lakini hawafanyi kazi kikamilifu,'' alisisitiza Komba.

Ametoa rai kwa maofisa elimu na wanaohusika kuchukua hatua na kwamba wanaoshindwa kusimamia elimu ameshauri wasihamishwe badala yake washushwe vyeo, na kwa kutoa mapendekezo kwa Mkurugenzi na kuletwa kwenye kikao cha madiwani ili kushughulikia nao.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji katika Baraza hilo, Manfred Mzuyu, alisema kamati yake ilifanya utafiti kwa kutembelea kata, baada ya matokeo mabaya ya elimu ya msingi na kubaini kuwa baadhi ya waratibu elimu kata, pikipiki walizopewa na serikali wanazitumia kwa matumizi yao na hawaishi kwenye vituo vyao vya kazi.

Diwani wa Kata ya Kizuka, Jacob Nditi, alisema, uchunguzi walioufanya wamebaini wasimamizi wa elimu wakiwamo waratibu elimu kata na walimu wakuu baadhi yao hawasimamii walimu ili kujua iwapo wanafundisha ipasavyo.



Mbunge wa Viti Maalum anayewakilisha kundi la asasi za kiraia (NGO) Tanzania Bara, Neema Lugangira, akichangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka (2021/2022), jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mashahidi 22 kujenga kesi ya kina Mdee

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayowakabili vigogo 26 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) akiwamo Halima Mdee dhidi ya kutoa lugha ya matusi na kuharibu geti la Magereza Segerea umedai mahakamani unatarajia kuita mashahidi 22 kuthibitisha mashtaka hayo.

Kadhalika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imepanga kuanza kisikiliza kesi hiyo mfululizo Aprili 5 mpaka 7, mwaka huu.

Kesi hiyo imesikilizwa maelezo ya awali jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Jamhuri ikiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Renatus Mkude alidai kuwa Machi 13, mwaka juzi, eneo la Gereza la Segerea wilayani Ilala, washtakiwa walifanya mkusanyiko usio halali katika namna ya kuleta hofu na kuvunja amani.

Alidai katika siku ya tukio washtakiwa walikaidi amri halali iliyotolewa na Ofisa wa Magereza B 3648 SGT John aliyewataka wasikusanyike eneo hilo, lakini hawakutii na kusababisha kuharibu geti la Magereza, kumjeruhi askari huyo na kumtolea maneno machafu. Mkude alidai washtakiwa wote ni raia wa Tanzania na wafuasi wa CHADEMA kabla ya tukio hilo, Mwenyekiti wa Chama hicho, Freeman Mbowe alitiwa hatiani kwa makosa mbalimbali na kupewa adhabu ya faini au kwenda jela.

Alidai Mbowe alishindwa kulipa faini na hivyo kwenda Segerea na kwamba utaratibu wa kulipa faini ulikuwa unaendelea.

Aliendelea kudai kuwa mshtakiwa Mdee, Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, Jesca Kishoa, aliyekuwa Meya wa Ubungo, Boniface Jacob walihamasisha washtakiwa hao kukusanyika Segerea ili kumpokea mwenyekiti wao.

# Ofisa mauzo asomewa shtaka la wizi mil. 89/-

**Na Hellen Mwango**

OFISA mauzo wa Kampuni ya Amsons Industries Tanzania Limited, John Mshana, amesomewa mashtaka yake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam dhidi ya wizi wa Sh. milioni 89.7.

Bosi huyo alisomewa mashtaka katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Wakili wa Serikali, Kija Luzungana, alidai kuwa kati ya Aprili 20, 2017 mpaka Machi 31, 2018 Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alitenda makosa hayo. Ilidaiwa kuwa mshtakiwa aliiba kiasi hicho cha fedha kupitia bidhaa alizokabidhiwa na mwajiri wake kwa ajili ya kuzisambaza kwa wateja.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana mashtaka yake.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Hakimu Chaungu alisema kesi hiyo itatajwa Machi Mosi, mwaka huu. Aidha, mahakama ilimtaka mshtakiwa kuwasilisha mahakamani fedha taslimu Sh.milioni 44.85 au hati ya mali isiyohamishika yenye thamani hiyo ya fedha.

Masharti mengine ni kuwa na wadhamini wawili watakaotia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni 22.4 kila mmoja, wenye barua za utambulisho, na akifanikiwa kutimiza masharti hayo, hatoruhusiwa kutoka nje ya mkoa wa Dar es Salaam bila kibali cha mahakama hiyo.

Mshtakiwa alishindwa kutimiza masharti hayo alirudishwa mahabusu.

# Wazazi wanaotumikisha watoto kiuchumi kusakwa

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MKUU wa Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Said Mtanda, amewaagiza watendaji kata na vijiji kuwakamata wazazi wanaowatumia watoto wao katika shughuli za kiuchumi badala ya kuwapeleka shule.

Shughuli za kiuchumi ambazo baadhi ya wazazi wanawatumia watoto wao ni kilimo, kuchunga mifugo na uvuvi.

Agizo hilo alilitoa jana wakati anazungumza na Nipashe lililotaka kujua kiwango cha wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wilayani humo wamefanikiwa kwa kiasi gani.

Alisema mpaka sasa wanafunzi walio ripoti katika shule walizopangiwa ni asilimia 80, huku wengine hawajaripoti na haijulikani walipo, na kwamba huenda wakawa wanatumikishwa katika shughuli za kiuchumi.

Alisema kutokana na hali hiyo, amewaagiza watendaji kata na vijiji kufanya msako katika maeneo yao, na ikiwa itabainika kuna wanafunzi hawaja ripoti shuleni wamkamatwe na mzazi wao ili wachukuliwe hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Alisema tangu uchaguzi wa wanafunzi hao ulipofanyika, ni muda mrefu umepita, hivyo serikali haiwezi kuendelea kuwa kimya, lazima ichukue hatua zichukuliwe kwa kuwa kunauwezekano mkubwa kwa wanafunzi hao wakapotelea mtaani na wasiendelee tena na shule.

## NMB yakabidhi madawati 50

**Na Mwandishi Wetu,** HANANG'

SHULE zilizopokea misaada inayotolewa na Benki ya NMB zimetakiwa kufanya vizuri katika masomo ili kuonyesha thamani ya misaada hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Ghibu Ringo, alipokuwa akizungumza baada ya kupokea msaada wa viti na meza 50 kwa ajili Shule ya Sekondari ya Getwanasi wilayani hapo.

Ringo alizitaka shule zilizopokea msaada kutoka NMB kuhakikisha wanafanya vizuri katika masomo na mitihani yao, ili kuonyesha thamani ya mchango huo.

"Unajua hata kama una mtoto wako unamlipia ada vizuri na kumnunulia mahitaji muhimu, unategemea kuona matokeo yake mazuri, sasa hata ninyi shule hii na wengine ambao wameshapokea misaada mbalimbali kutoka NMB nataka kuona mnaonyesha mafanikio zaidi katika masomo yaenu," alisema.

Alisema lazima wanaopata misaada hiyo kutoka benki hiyo na wadau wengine wa elimu na maendeleo kuonyesha thamani ya fedha zinazotolewa ili kuwatia moyo wa kuendelea kuwapa wengine.

Aidha, aliwataka wakuu wa shule na kamati za shule kuweka mikakati ya kuvitunza vifaa vinavyotolewa na wadau wa maendeleo.

Alisema misaada inapotoka inarekodiwa vizuri na uongozi wa halmashauri, hivyo haiwezekani shule hiyo hiyo kuendelea kuomba msaada wa vifaa hivyo.

Naye Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Hanang, Solomon Shati, alisema halmashauri hiyo inazo shule za sekondari 36 na kati ya shule hizo ya binafsi ni moja tu.

Alisema kati ya shule hizo za serikali benki ya NMB imetoa misaada kwa shule mbili kwa mwaka jana na mwaka huu, ambapo msaada huo umesaidia kuleta mabadiliko kwa kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Rose Kamili, alisema misaada ya benki hiyo imekuwa ikilenga maeneo ya wananchi wa uchumi wa chini, jambo ambalo limekuwa likiigusa jamii.

Kwa upande wake Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema msaada huo unathamani ya Sh. milioni tano na unatokana na gawio la faida iliyopata benki na kuirushia jamii kutokana na kuwaunga mkono.




Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Ghaibu Ringo (katikati), Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (kushoto) na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hanang, Rose Kamili, wakiwa wamekaa kwenye madawati yaliyotolewa na Benki ya NMB kwa Shule ya Sekondari Getwanasi mkoani Manyara, yenye thamani ya Sh. milioni tano. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Coca-Cola Kwanza kutambua mwanamke shujaa

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya vinywaji ya Coca-Cola Kwanza, imezindua kampeni ya kumtambua mwanamke shujaa kwa lengo la kutambua mchango mkubwa unaofanywa na wanawake hao katika kuliletea taifa maendeleo.

Imezindua kampeni hiyo ikiwa ni maandalizi ya kuelekea Siku ya Wanawake Duniani ambayo huadhimishwa Machi 3, kila mwaka.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara na Mauzo Coca-Cola Kwanza, Josephine Msalilwa, alisema lengo la kampeni hiyo ni kusherehekea, kutambua na kuhamasisha wanawake kutoka katika sekta mbalimbali kuendelea kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Pia, alisema katika kutambua mchango kwa wanawake hao, watatoa tuzo kwa wanawake wanaofanya vizuri katika sekta mbalimbali hususani katika nafasi za uongozi.

"Kampeni hiyo ambayo imebeba kaulimbiu ya "Mwanamke shujaa", inakusudia kutambua juhudi zao, kujenga uwezo kwa wanawake wenyewe kuhamasishana katika maendeleo, kujijengea ujasiri wa kujenga uhusiano kwa watu waliofanikiwa na hata kufikia usawa wa kijinsia kwa maendeleo endelevu," alisema Msalilwa.

"Siku hii kwa mwaka huu pia inazingatia wanawake katika uongozi, na Coca-Cola Kwanza kwa kutambua juhudi wanazofanya imeamua kuzindua tuzo inayojulikana kama Excellence in Leadership Awards na tumepanga kuitoa kwa wanawake walio katika nafasi za uongozi kutoka katika sekta 10 tofauti."

Mratibu wa kampeni hiyo, Yvette Gadi, alisema upo umuhimu mkubwa kwa mwanamke kushiriki kikamilifu kwenye vyombo vya maamuzi.

Sarah Pima, ambaye ndio jaji mkuu wa kampeni hiyo alisema tuzo zitakazotolewa kwa wanawake hao ni za uongozi wa elimu, uongozi wa michezo, biashara na ujasiriamali, uongozi katika sekta ya afya, sayansi na teknolojia na katika sekta ya utalii.

Nyingine ni katika jamii na utamaduni, uongozi wa vyombo vya habari, burudani na uongozi wa biashara ya kilimo.

# Athari za ukeketaji zabainishwa

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZEA kuwa ukeketaji unaendelea katika baadhi ya maeneo, umekuwa ukileta madhara ya kiafya kwa waliofanyiwa, wakiwamo watoto kupoteza mwelekeo wa masomo darasani.

Mbali na kufanya vibaya katika taaluma, pia watoto hao wamekuwa na woga kiasi cha kutokwenda kucheza na wenzao.

Hayo yalisemwa na Mathew Suleiman, mwalimu wa Shule ya Sekondari Misitu, iliyopo Kitunda jijini Dar es Salaam.

"Ukeketaji unapofanywa kwa wanafunzi, umekuwa ukichangia wanafunzi kupoteza mwelekeo na kusababisha pia kufanya vibaya kitaaluma," alisema.

Mwalimu Mathew alisema elimu iendelee kutolewa kwa jamii, ili wachukie matukio ya ukeketaji na ukatili.

Joseph Mapunda, Mchungaji wa Kanisa la Assemblies of God, ambaye alishiriki kutoa elimu ya ukeketaji katika maeneo ya Kitunda na Kivule, alisema ukeketaji haupo katika dini bali kinachofanywa ni tohara kwa watoto wa kiume.

Mapunda aliongeza wote wanaokeketa wanawake wanakiuka kwa kuwa wanawapunguzia viungo wenzao, ambavyo Mungu aliwapatia. Aliupongeza Mtandao wa Jinsia Tanzaniua (TGNP) kwa kuitumia siku ya ukeketaji kwa kwenda maeneo mbalimbali kutoa elimu kwa jamii, itakuwa mkombozi kwa jamii. Pia aliitaka jamii isiwafumbie macho watu wanaokeketa na kwamba wawaripoti ili wachukuliwe hatua.

Hellen Urio, mratibu wa miradi wa TGNP, alisema mtandao huo umejikita katika mambo matano, ambayo ni maji, elimu, afya, mwanamke kumiliki ardhi na vitendo vya ukatili na ukeketaji.

Alisema wanafanya kazi na vituo vya maarifa na taarifa, ambapo kuna jamii inapata fursa kupitia vituo hivyo.

Alisema kupitia matukio ya ukeketaji, wamekuwa wakitoa elimu hiyo ili mabinti nao wasi-



Wasafirishaji wa mizingo midogo wakisubiri wateja katika soko la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. Soko hilo kipindi cha mvua linachangamoto ya matope. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# RC ataka taarifa polisi kwa wakati

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ametoa wito kwa wakazi wa mkoa huo, kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za matukio mbalimbali kwa Jeshi la Polisi ili liweze kushughulikia kwa wakati.

Ndikilo alitoa wito huo juzi, alipokuwa akipokea madawati 50 yenye thamani ya Sh. milioni 4.8 kutoka Jeshi la Polisi mkoani Pwani.

"Nimefurahi kwamba pamoja na kutoa madawati, lakini mmesema ili Jeshi la Polisi liweze kufanya kazi vizuri mnachohitaji ni taarifa, niendelee kuwahimiza wananchi wa Mkoa wa Pwani kwamba ili Jeshi la Polisi liwasaidie kwa ufanisi mkubwa basi toeni taarifa," alisema Ndikilo.

Alishukuru jeshi hilo kwa kuthamini elimu na kuchangia madawati hayo ambayo yataondoa kero ya wanafunzi kukaa chini. Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema madawati hayo yametolewa kutimiza ahadi waliyoitoa Januari 29, mwaka huu.

Wankyo alisema jeshi hilo liliahidi kuchangia madawati 50 ya shule za sekondari ili kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani tunatoa mchango huu tukitambua kuwa sisi ni sehemu ya jamii na pia ni wazazi, tunaomba wananchi wote mwendelee kutuunga mkono katika juhudi za kupambana na kuzuia uhalifu."

Wankyo alisema ili jeshi hilo lifanye kazi kwa weledi linahitaji ushirikiano wa taarifa zinazohusika uhalifu wazifanyie kazi na mkoa uendelee kuwa salama.

# Walimu wapewa angalizo tamaa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

OFISA Elimu Mkoa wa Rukwa, Abel Ntupa, amewaonya walimu wakuu wa shule za msingi na waratibu elimu kata katika mikoa ya Rukwa na Katavi kuacha tamaa kwa kuwa imekuwa kikwazo kikubwa katika kutekeleza majukumu yao.

Onyo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Rukwa, wakati akimwakilisha katibu tawala wa mkoa huo, kufunga mafunzo ya siku tatu ya udhibiti ubora wa ndani kwa walimu wakuu wa shule za msingi wa mikoa hiyo yaliyofanyika katika Chuo cha Ualimu Sumbawanga.

Alisema serikali katika kuwarahisishia mazingira ya kazi maofisa elimu kata, iliamua kutoa pikipiki kwa baadhi yao kama kitendea kazi, lakini baadhi yao wamekuwa wakiziweka vijiweni na kuzitumia kama bodaboda ili wajipatie kipato.

Alisema serikali imekuwa ikiwapa watumishi hao mishahara, posho ya madaraka na stahiki nyinginezo, lakini wamekuwa na tamaa mbaya kiasi cha kuchukua pikipiki hizo na kuanza kuzitumia kwa kutafuta fedha. "Kuna baadhi ya waratibu elimu kata walipewa pikipiki na serikali ikiwa ni kitendea kazi, lakini cha kusikitisha wamekuwa wakizitumia kwa kuziweka vijiweni na kuzikodisha kama bodaboda, hii ni tamaa mbaya," alisema.

"Baadhi ya walimu wanatamaa mbaya, unakuta mwalimu analima mpaka anapata gunia 150 za mahindi, zote hizo za nini? Ndio maana wakulima wanakosa soko la mazao yao, wewe una mshahara, posho ya madaraka na marupurupu mengine, unalima na kupata gunia 150 na kazini kwako unawajibika kweli?" Alihoji na kuendelea:

" Unapata muda saa ngapi wa kusimamia mashamba, ndio maana mkikaguliwa mnapata wastani wa E."

Awali akisoma taarifa ya mafunzo hayo Mratibu wa Mafunzo kutoka Chuo cha Uongozi ADEM, Fravian Mbaga, alisema mafunzo hayo ni mahususi kwa ajili ya kuwajengea walimu wakuu uwezo wa kusimamia ubora wa shule. Alisema kuwa jumla ya walimu 271 kutoka halmashauri tisa za mikoa hiyo wamehudhuria kwa asilimia 100, na kwamba ni matumaini yake wataweza kutumia mafunzo hayo kuleta tija katika sekta ya elimu katika mikoa hiyo.

Dk. Joanes Balige, kutoka ofisi ya Rais (TAMISEMI) idara ya usimamizi wa elimu, alisema walimu wanapaswa kujituma zaidi katika utendaji kazi na wahakikishe wanautumia mtaala uliopo na wafikie malengo ya serikali kwa asilimia 100, kwani mtaala uliopo ni bora na unafaa kwa elimu.

# Ruvuma yakoshwa elimu bila malipo

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MKOA wa Ruvuma umepokea Sh. 9,205,781,600.28 ili kutekeleza sera ya utoaji elimu bila malipo katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Desemba 2019 hadi Novemba 2020.

Mkuu wa Mkoa huo, Christina Mndeme, amesema fedha hizo zimesaidia kuongeza kiwango cha uandikishaji na mahudhurio ya wanafunzi katika shule za msingi na sekondari pamoja na kuongezeka upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada.

"Utekelezaji wa sera hii umeweza kuleta unafuu kwa wazazi na walezi katika kugharamia gharama za elimu kwa watoto wao," alisisitiza Mndeme.

Alisema mkoa umeendelea kuimarisha utoaji wa elimu katika ngazi zote, na kwamba umepata mafanikio makubwa baada ya serikali kujenga vyuo viwili vipya vya Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA) na kuufanya Mkoa kuwa na vyuo vitatu vya VETA.

Kwa mujibu wa Mndeme, mkoa hivi sasa unaweka msukumo mkubwa katika kuimarisha utoaji wa taaluma bora kwa kuwashirikisha wadau wote wa elimu ili kuhakikisha kila mdau anashiriki kufanikisha ufundishaji, ujifunzaji na mahudhurio ya wanafunzi shuleni.

Aliishukuru serikali kwa kuendelea kufanya elimu kuwa kipaumbele.

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya shule za msingi 808 kati ya hizo, shule za serikali ni 778 na zisizo za serikali 30, pia mkoa una shule za sekondari 206, kati ya hizo za serikali ni 150 na sekondari binafsi 56.



Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa (wapili kushoto), akiwa kwenye mahojiano na wafanyabiashara wa soko kuu la Morogoro pamoja watendaji na viongozi mbalimbali wa manispaa wakati wa zoezi la uhakiki. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Waomba majengo kituo cha afya kutumika

**Na Jumaqnne Juma,** MULEBA

WANANCHI Kata ya Ijumbi wilayani Muleba, mkoani Kagera, wameomba serikali kuharakisha matumizi ya majengo matatu yaliyokabidhiwa kwa halmashauri kwa ajili ya matumizi ya kituo cha

afya, ili waweze kupata huduma ya matibabu kwenye kata hiyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi na viongozi wa eneo hilo, walisema kukosekana kwa huduma za afya kwenye kata yao kunawapa shida kutafuta umbali mrefu.

Akizungumza kwa niaba ya wanakijiji wenzake, Petruinda Rwiza, alisema

uwepo wa kituo hicho utawaondolea changamoto ya kutembea umbali mrefu

kufuata huduma za afya katika hospitali teule ya wilaya Rubya.

"Si hivyo tu bali itatusaidia kupata huduma za dharura hasa pale mtu anaposhikwa ugonjwa ghafla nyakati za usiku," alisema.

Naye Diwani wa Kata ya Ijumbi, Wilbard Musirigi, alisema majengo matatu yalitolewa na Mfadhili Prosper Rweyendera mwaka 2019

kwa ajili ya kituo cha afya, lakini yakihitaji ukarabati wa miundombinu ili kuyaweka katika mfumo wa kituo cha afya.

"Katika bajeti ya mwaka 2020/2021 serikali ilitenga Sh. milioni 50 kwa ajili ya kukarabati majengo mawili, kujenga kichomea taka, nyumba ya mganga na chumba cha upasuaji," alisema.

"Kwa mwaka huu ukarabati utafanyika pamoja na kukisajili kituo, mahitaji ya huduma ya afya ni makubwa kwani kati ya kata sita zinazokizunguka kijiji cha Rubao ni kata moja yenye zahanati, kata zote zinategemea huduma kutoka kwenye kituo hicho kikianza kutoa huduma," alibainisha.

Naye Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Salehe Mruma, alisema kwa sasa majengo hayo yanatumika kwa ajili ya kliniki ya mama na mtoto.

Alisema vijiji viwili vinapata huduma hiyo Ijumbi na wananchi wengine kutoka maeneo mengine kila mwezi na watumishi wa kutoa huduma wanafika kituoni hapo kwa ratiba.

Aidha, Salehe aliomba aliyewafadhili majengo asichoke kufanya hivyo kwani mahitaji bado ni mengi, baadhi ya miundombinu inaweza kuchelewa,

anaweza kutusaidia hayo mahitaji ili kukamilisha haraka ukarabati.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji huyo, alisaini mkataba wa kukabidhiwa majengo hayo pamoja na Diwani Musirigi mwaka 2019 na makabidhiano yalikuwa kati ya Prosper Rweyendera ambaye ni mmiliki wa majengo na Halmashauri ya Muleba pamoja na Halmashauri ya Kijiji cha Rubao.

Majengo hayo yenye thamani ya Sh. 149,442,531 yalikabidhiwa bure kwa makubaliano kwamba yaanze kutumika kutoa huduma za afya ndani ya miaka mitatu.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Modest Rwakehemura, akizungumzia kituo hicho cha afya alisema ukarabati wa majengo utaanza hivi karibuni na huduma rasmi zitaanza mwaka ujao wa fedha (2021/22).

Alisema kwa kuanzia, kituo kitatoa huduma za upasuaji wa dharura kwa mama wajawazito na zingine zote zinazohusu mama na mtoto.

"Tunazingatia pia mahitaji ya chumba cha upasuaji kwa huduma zaidi za upasuaji. Tutakuwa tukiimarisha huduma kwa awamu kulingana na

bajeti inavyoruhusu. Vilevile tunashukuru kwamba wadau wengine wanajitokeza kuuunga mkono juhudi za mfadhili wa kwanza aliyetupatia majengo haya matatu," alibainisha.

## Serikali yasaidia ujenzi vyumba vya madarasa

**Na Yasmine Protace,**
KIBAHA

WAKAZI wa Kijiji cha Kitomondo, wilayani Kibaha Mkoa wa Pwani wameipongeza serikali kwa kuwapelekea Sh. milioni 60 za kujenga madarasa matatu kwenye Shule ya Msingi Kitomondo.

Akizungumza kwenye ziara ya Mbunge wa Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo, kukagua miradi ya maendeleo, Diwani wa Kata ya Ruvu, Shaban Chamba, alisema pamoja na pongezi hizo, wananchi wa kijiji cha Minazi Mikinda wametenga eneo la kujenga shule ya msingi na wapo tayari kushirikiana naye jengo hilo lifikie hatua ya boma, huku naye akiahidi kupiga kambi hapo ili kutimiza malengo hayo yenye tija kwa maendeleo ya watoto.

Mbunge huyo ambaye ni mzaliwa wa Kata ya Ruvu, alisema mkakati huo utaenda sambamba na ujenzi wa hosteli shuleni Kitomondo ili kuwaokoa wanafunzi hususan wasichana kutembea umbali mrefu.

Mwakamo aliyeongozana na madiwani wa viti maalumu Halmashauri ya Kibaha Vijijini, aliwahakikishia wananchi kuwa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Kibaha hivi karibuni utaanza kujenga barabara imara kutoka Mkino hadi Kitomondo yenye urefu wa kilometa 12, ambayo ni fursa kwa wafanyabiashara wa mifugo na wawekezaji mbalimbali kuhamia hapo kutokana na uwapo wa ardhi ya kutosha.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Vijijini, Erasto Makala, alipongeza utamaduni wa mbunge huyo kushirikiana na madiwani pia na wataalamu kutatua changamoto za wananchi vijijini kwenye sekta

Nipashe
TESA
Jumanne Februari 16, 2021
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12

Mgodi wa dhahabu uliogeuka adhabu



Ukurasa 14

## Shule ilivyovuna maajabu baada ya kutunza misitu

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# KITISHO VIRUSI CORONA

- Hubadilika kila uchao, chanzo chanjo kudunda
- Aina mpya hatari ipo Brazil, husambaa na kuua fasta

KIRUSI cha corona kilichoanza kushambulia dunia mwishoni mwa mwaka 2020 kinawaweka watu kwenye mazingira ya hofu zaidi, kutokana na kubadilika mara kwa mara na kujiimarisha kiasi cha kuidhoofisha kinga ya mwili na pia kuzidi kuwa ngangari kwa chanjo zinazotengenezwa.

Virusi vya corona vinajulikana kusababisha magonjwa yanayoshambulia njia za hewa, kuleta homa kali na kusimamisha upumuaji, vichomi na maumivu makali, kooni, kifuani na kwenye mbavu. Hali inapozidi kuwa mbaya mgonjwa analazimika kutumia mashine ya kusaidia kusukuma hewa mapafuni.

Kinachoripotiwa sasa ni mabadiliko ya virusi hivyo ambavyo kitaalamu huitwa 'mutation' ambayo hufanyika kwenye mfumo wa nasaba za kirusi, hivyo kubadilisha namna kilivyokuwa hapo awali na kukipa sura nyingine mpya ikiwa ni pamoja na kuwa na afya na nguvu zaidi.

Kwa mujibu wa taarifa za mitandao virusi vya corona mwanzoni vilijulikana kama COVID-19 na viliripotiwa nchini China kwenye Jimbo la Wuhan. Lakini baada ya kusambaa sehemu mbalimbali duniani kimekuja na sura mpya na kinachoogopesha ni wadudu hao kuwa na kasi ya kushambulia na uwezo wa kuua haraka zaidi kuliko ilivyokuwa kwa COVID-19.

Taarifa hizo zinasema virusi vipya vinaibuka na kutoweka, lakini vipo vinavyodumu na kuendelea kudumu, kushika kasi na kuwa na nguvu zaidi kama ambavyo inatokea sasa na kwa upande wa corona virusi vipya vimeripotiwa nchini Marekani, Uingereza na Afrika Kusini.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linakiri kuwa kiwango kikubwa cha virusi vya corona kinasambaa sehemu mbalimbali na kinabadilika na hivi karibuni utoaji wa chanjo sehemu mbalimbali ulisitishwa kutokana na ukweli kuwa kirusi kimejiimarisha zaidi na hakiwezi kudhibitiwa kwa kuwachanja watu dawa ya chanjo mathalani ya AstraZeneca.

Hivi karibuni Afrika Kusini ilisitisha utoaji wa chanjo hiyo iliyotengenezwa na kampuni za dawa za Uingereza na Sweden (British-Swedish) baada ya kugundulika kuwa haiwezi kuwa mwarobaini wa COVID-19 kwa vile kirusi kimebadilika na kuwa na sura na nguvu kubwa tofauti na hapo awali.



Chanjo ya COVID-19 iliyokataliwa Afrika Kusini ni baada ya kubainika kuwa haiwezi kukabiliana na aina mpya ya virusi vya corona vilivyoibuka mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

### VIRUSI VILIVYOIBUKA

Nchini Uingereza kirusi kipya kilichopewa jina la 'B.1.1.7' kiliripotiwa kuonekana miongoni mwa wagonjwa kikielezwa kuwa na uwezo mkubwa wa kujibadilisha na kujiimarisha zaidi hali iliyogundulika kuanzia mwishoni mwa 2020. Kirusi hicho kina sifa ya kusambaa kwa kasi kubwa na kushambulia haraka zaidi kikilinganishwa na jamii nyingine hasa COVID-19.

Januari mwaka huu wataalamu wa Uingereza waliripoti kuwa waligundua kuwa kirusi hicho kipya kina uwezo wa kuua kwa haraka kuliko kile cha awali na kwamba zilihitajika tafiti zaidi kuthibitisha maelezo hayo. Jamii hiyo iligundulika sehemu nyingine nyingi duniani na kwa Marekani kilionekana Desemba 2020.

Huko Afrika Kusini kirusi kingine kilichopewa jina la 'B.1.351' kiliibuka kutoka kwenye jamii ya 'B.1.1.7' ambacho kiliripotiwa UIngereza. Baada ya kukitambua wataalamu wa elimu ya virusi walisema walikigundua Oktoba 2020 na kwamba virusi aina ya 'B.1.351' wana sifa zinazolingana na kufanana na kirusi 'B.1.1.7,' chenye asili ya Uingereza. Baadhi ya wagonjwa wenye kirusi hicho walipatikana pia nchini Marekani mwezi uliopita.

Nchini Brazil kirusi kipya cha corona kilipewa jila la 'P.1' ambacho kwa mara ya kwanza kiliripotiwa kuwa kilipatikana miongoni mwa wasafiri waliotoka Brazil waliofanyiwa vipimo katika moja ya viwanja vya ndege vya Japan mwezi uliopita.

Wataalamu wa virusi walivielezea kuwa ni 'P.1' ambacho ni zao la mabadiliko au 'mutation' ambacho kina tabia mpya zinazopiga chenga kinga ya mwili na kuizuia isivitambue na hivyo kujiimarisha na kuudhoofisha mwili ambao unakosa taarifa za kuwapo kwa kirusi hicho mwilini na kuongeza ugumu wa kupambana nacho.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa utafiti umeonyesha kuwa kuwapo kwa kirusi hicho kipya jamii ya Brazil kumeongeza kasi ya kusambaa maradhi ya corona duniani na kwamba uharaka wa kuenea ni mkubwa kuliko virusi vingine. Yote hayo yanaongeza hofu ya uwezekano wa kuwa na wagonjwa wengi zaidi ambao ni mzigo mzito kwa sekta ya afya, kununua dawa na kugharamia matibabu yote hayo yakiongeza idadi ya wagonjwa hospitalini na idadi kubwa ya vifo vinavyoongeza hofu ya hatima ya maisha.

Matumizi ya barakoa, kukaa umbali wa zaidi ya mita moja, kunawa mikono mara kwa mara, kutumia vitakasa mikono na kujiweka karantini ni miongoni mwa mikakati inayoweza kupunguza kasi ya kuendelea kusambaa virusi vya COVID-19 na jamii mpya inayoibuka kutokana na kujibadilisha nasaba. **MTANDAO**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mgodi wa dhahabu uliogeuka adhabu

• Mikataba huandikwa kwa lugha isiyofahamika • Hulipua miamba wachimbaji wakiwa migodini • DC, OSHA, watoa maagizo lakini watumishi...

PENGINE ni tatizo la wafanyakazi na waajiri kutoa sheria za kazi au kuzipuuza ama kudharau. Yote yanaweza kuwa maelezo ya kuzungumzia kile kinachoendelea kujiri kwenye moja ya migodi ya dhahabu iliyoo mkoani Shinyanga.

Wakati hayo yanatokea hivi karibuni serikali ilieleza azma yake ya kuelimisha wananchi kuhusu Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya Mwaka 2004, ikiwa ni mikakati ya kusaidia wafanyakazi na wawekezaji kuwa na uhusiano mwema kazini na serikali kunufaika ikapata kodi, huku kukiwa na amani kutokana na uwapo wa ajira zenye staha.

Eneo mojawapo linalowasumbua waajiriwa ni kwenye sekta ya madini ambalo kila wakati kumekuwa na malalamiko ya wafanyakazi na vibarua na hata jamii zinazowazunguka wawekezaji hao, kwa vile wanaoishi sehemu hizo wanadai wanakuwa na changamoto kuanzia za kukosa ajira na kunyimwa fursa za kutoa huduma mbalimbali ndani ya migodi na unyanyasaji.

Serikali inapoamua kuelimisha umma kuhusu sheria ya ajira na mahusiano kazini ya 2004 mgodi wa ZEMD unaomilikiwa na wawekezaji wa kigeni wanaochimba dhahabu katika eneo la Mahiga wilayani Shinyanga, wafanyakazi wake wanaomba ianzie kwao. Wakiamini kuwa ni eneo la kutembelewa kutokana na manyanyaso mbalimbali.

Wakazi wa Mahiga hasa wachimbaji wanaona kuwa mgodi umekuwa shubiri na wala si neema kwa wenyeji wanaouzunguka licha ya kuwapatia ajira vijana wa sehemu hiyo, wanataja mazingira hatarishi ya kazi na kutojali uhai kuwa ni mambo yanayowafanya kuiona kuwa hawana bahati licha ya kuwa na ajira.

Wachimbaji wanasema hufanyakazi bila vifaa kinga, huku wakilazimishwa kuzama kwenye migodi wakati ulipuaji wa miamba ya mawe ya madini ukiendelea, licha ya kuwapo moshi wenye sumu tena hakuna hewa ya kutosha na wanapotoka nje hufokewa na kuambiwa warudi chini ya ardhi kuendelea na kazi.

"Kwenye mgodi huu tunafanya kazi kwa sababu hatuna ajira, lakini si mahali salama tunasikitika kuwa wawekezaji hawa wageni hawasogei kwenye maeneo hatarishi na hawajali kutupatia vifaa kinga na kila unapozungumzia suala la staha kazini unatishiwa kutufukuza kazi," anasema mmoja wa wachimbaji.

"Juzi tungekufa wakati wamiliki wakilipua miamba kwa baruti. Ulitoka moshi wenye sumu ukatuzidi na wenzangu wawili waliishiwa nguvu na kuzimia, ikabidi niwapandishe kwenye viberenge vya kutolea mawe yenye dhahabu kinyume na utaratibu, ndipo tukatoka nje," anasema mchimbaji aliyenusurika kwenye kadhia hiyo.

Philibert Elisha ni mchimbaji mwingine anayezungumzia kukosekana ajira zenye staha akisema: "Kukosa vifaa kinga kumesababish nipondwe na jiwe wakati wa kulipua miamba na hili liliniumiza mgongo na mguu, na baada ya kupata ulemavu huo wawekezaji hawa wageni walininyima fedha za matibabu na kunifukuza kazi kwa maelezo kuwa ni mwenye ulemavu siweza kufanya kazi tena."

Anasema wanapoomba vifaa hivyo huambiwa kama hawataki kazi waache, kwani kuna watu wengi wapo getini kila siku wanaomba kazi, na hivyo kulazimika kufanyakazi katika mazingira hayo hatarishi sababu ya kutetea ajira.

"Unaponiona hapa na chechemea ni sababu ya kupondwa na mawe wakati wa upasuaji miamba na nilikuwa sijavaa vifaa kinga, na wapo vijana wengi tu wameshapata ulemavu kupitia huu mgodi, wamesharudi majumbani mwao kujiuguza, tuna nyanyasika sana na mimi nilishafukuzwa sina kazi tena," anasema Elisha.

Juma Gambaliko anasema kutokana na manyanyaso kwenye mgodi huo, hawapewi hata maji ya kunywa, hasa wale ambao wanazama chini kupasua miamba ya dhahabu na hatimaye hujikuta wakinywa maji yenye sumu ambayo hutiririka chini yakiwa na kemikali.

"Waajiri wetu hawana huruma hawajali ubinadamu licha ya kwamba hatupewi maji ya kunywa na haturusiwi kutoka nje ya shimo hadi saa za kazi ziishe," anasema Gambaliko.

"Na hapa mgodini wanapofika wataalamu kutupima afya zetu wengi wetu ni wagonjwa, tunakohoa, kuumwa, vichwa na matibabu ni shida na ukizidiwa unarudishwa kwenu siku ukipona ndipo unaruhusiswa kuendelea na kazi," anaongeza.



Wawekezaji wanatarajiwa kutumia teknolojia ya kisasa badala ya kuendeleza uchimbaji unaotegemea zana za kizamani kama sururu na kulipua miamba kwa baruti bila kuzingatia usalama wa maisha ya wafanyakazi wao. **PICHA: MTANDAO**

> "Waajiri wetu hawana huruma hawajali ubinadamu licha ya kwamba hatupewi maji ya kunywa na haturusiwi kutoka nje ya shimo hadi saa za kazi ziishe.

### MIKATABA TATA

Teddy Malima ni mtaalamu wa vilipuzi au baruti kwenye mgodi huo anasema wamekuwa wakiomba hata barakoa kwa ajili ya kujikinga na vumbi na kemikali, lakini hawapewi huku vitambulisho vyao vya kazi vikiandikwa kuwa ni wapishi. Mikataba isiyo bayana na mara nyingi hawatendewi haki.

Benard Mwihambe anaongeza: "Unapoomba kazi mgodi hapa unapewa mikataba na kuisaini kwa muda mfupi bila ya kuisoma kwani imeandikwa Kichina na Kiingereza. Unalazimishwa kuisaini bila ya kujua kiwango cha mshahara..."

Anasema mikataba ambayo wanapewa kwenye mgodi huo ina maswali mengi mojawapo ni kukatwa makato ya mifuko ya hifadhi ya jamii bila ya kupewa namba za uanachama na hawajui kiwango cha makato hayo, pamoja na kukatwa kodi nyingine bila kupewa risiti.

### UKAGUZI WA DC

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga Jasinta Mboneko, baada ya kupokea malalamiko ya manyanyaso ya wafanyakazi kwenye mgodi huo, analazika kufanya ziara ya kwenda kujionea hali halisi, na kukutana na wafanyakazi wanaochechemea sababu ya kupata ajali kwenye mgodi huo kutokana na kukosa vifaa mbalimbali.

Anasema serikali inapenda wawekezaji, lakini inawataka wafuate sheria zikiwamo za uchimbaji, usalama, afya, na utunzaji wa mazingira, na siyo mgodi kugeuka kuwa eneo la kusulubisha Watanzania, bali uwe sehemu ya kubadilisha mfumo wa maisha yao ili yawe bora.

"Fuateni sheria za nchi na taratibu zote zilizowekwa na siyo kunyanyasa wafanyakazi ambao ni Watanzania, nimefanya ziara hapa ili kuwekana sawa, sababu kama hakuna amani kwenye mgodi huu, basi haina haja ya nyie wawekezaji kuendelea kuwapo," anasema Mboneko.

"Nafahamu sisi ni marafiki, lakini nyie mnachokifanya hapa kwa wafanyakazi wenu si sahihi kabisa bali fanyeni kazi katika mazingira rafiki ili na hawa watumishi wenu licha ya kupata ajira nao wafurahie kazi yao na siyo kuwanyanyasa," anaongeza.

Anatoa mwezi mmoja kwa uongozi wa mgodi huo, kufanyiakazi upungufu wote ambao umejitokeza, kwa kuzingatia maelekezo ya OSHA, na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na kuzitaka taasisi hizo kutembelea mgodi na kumaliza changamoto zote ili kuwapo na usalama na amani kwa wafanyakazi.

Mkuu wa Wilaya aliutaka mgodi huo kuajiri mtu ambaye atakuwa akisikiliza kero za wafanyakazi na kisha kuziwasilisha kwa viongozi wa mgodi na kutafutiwa ufumbuzi, kuliko hivi sasa wanaisha bila ya kuwapo kwa mtumishi huyo wa kuwasemea shida zao.

### MAELEZO YA SERIKALI

Kaimu Meneja wa Wakala wa Usalama na Afya Kazini (OSHA) Kanda ya Ziwa, Mjawa Shenduli, anapoulizwa kuhusu malalamiko ya wafanyakazi anasema walishindwa kuwapiga faini wamiliki wa mgodi ili fedha hizo zitekeleze maagizo waliyowapa wamiliki, lakini wanashangaa hakuna mabadiliko.

Anasema unapoanzisha mgodi lazima ufanye kwanza tathmini ya vihatarishi katika sehemu za kazi, lakini ZEMD haijafanya hivyo, bali umeanza shughuli za uchimbaji madini bila ya kufuata taratibu za kiusalama na afya.

"Mwaka 2020 tulifika kufanya ukaguzi, tukakuta una mapungufu mengi sana, hivyo ikabidi tusitishe kwanza kuwapiga faini, ili fedha hizo ambazo tungewapiga faini wazitumie kufanya marekebisho yaliyopo, lakini hakuna utekelezaji wowote uliofanyika huku wafanyakazi wakiendelea kuumia," anasema Shenduli.

"Pia kisheria wale wafanyakazi ambao wamepata ajali kwenye mgodi huu, tulipaswa kupewa taarifa ili tufike tufanye uchunguzi, lakini hatukuelezwa. Wanafanya makosa, na hili tunatoa onyo la mwisho kwao, tofauti na hapo tutawapiga faini," anaongeza mkaguzi huyo.

Anasema mgodi huo ulipaswa kuwapima kwanza afya wafanyakazi wake na wakati wakiendelea na kazi pia wapimwe afya na mikataba inapokwisha na kutaka kuacha kazi wanapaswa kupimwa tena afya, lakini mgodi huo haufanyi hivyo na kuonya kuwa ni kukiuka sheria za nchi.

Pia anafafanua kuwa mwaka huu lazima watakwenda na wataalamu wa afya kwenye mgodi huo kwa ajili ya kupima wafanyakazi na kubainisha magonjwa yatokanayo na vumbi lenye sumu na kusisitiza umuhimu wa kupewa vifaa kinga.

### OFISI ZA MADINI

Ofisa Madini mkoani Shinyanga, Camilius Seneda, anapozungumzia changamoto ya kulipua miamba anasema mgodi huo umekeuka sheria za uchimbaji madini, ambapo kwenye suala la kulipua miamba wanapaswa wafanyakazi wote watoke nje ya mashimo ili wasidhurike na vumbi lenye sumu pamoja moshi wa baruti lakini wao hawafanyi hivyo.

Anasema kitaalamu kwenye suala la kulipua baruti lazima kuwapo na mawasiliano kati ya watu waliopo ndani ya shimo na waliopo nje na baruti zikishalipuliwa hakuna anayeruhusiwa kuingia ndani hadi vumbi lenye sumu liishe mchakato unaochukua saa 1:30.

### UTATA MIKATABA

Ofisa Kazi Mkoani Shinyanga, Revocutus Mabula, anasema kwenye mgodi huo walishatoa maelekezo namna ya kufuata taratibu za kazi, ikiwamo kutoa mikataba ya mwaka mmoja na iwe imeandikwa kwa Kiingereza na Kiswahili, pamoja na kuacha kuwasainisha bila ya kuusoma na bila kufahamu kiwango cha mshahara.

Akizungumzia suala la NSSF, alisema lazima wafanyakazi hao wawe na namba za uanachama pamoja na kujua kiwango cha fedha sahihi za makato na siyo kukatwa kienyeji pamoja na kupewa pesa mkononi za mshahara ambao hauna kiwango maalumu, bali wanapaswa kulipwa kupitia akaunti za benki.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Shinyanga Godson Mwanawima, anaahidi kuwa idara hiyo itakwenda kufanya uchuguzi wa kina juu ya taarifa ambazo wanazipata za wawekezaji hao wa mgodi huo za kuwapo vitendo vya unyanyasaji wa wafanyakazi na ikibainika itabidi wachukue hatua za kisheria kutokana na kuwakandamiza Watanzania.

"Idara ya Uhamiaji Mkoa Shinyanga, tutakwenda kwenye mgodi huo kufanya uchunguzi juu ya malalamiko ya wafanyakazi kunyanyaswa na wawekezaji hawa ambao ni raia wa kigeni kwanza tunasikia wapo 60, lakini kwa taarifa tulizonazo uhamiaji wapo 20, hawa 40 waliingiaje hapa nchini?" Anahoji Mwanawima.

### ZEMD WANASEMAJE?

Meneja Msaidizi wa Mgodi wa ZEMD Zhao Chao, raia wa China, anakiri kuwapo na upungufu huo, na kubainisha kuwa maelekezo yote yaliyotolewa na serikali yatayafanyia kazi, ili wafanyakazi wawepo kwenye mazingira salama, kwa mujibu wa taratibu za sheria za uchimbaji madini na usalama mahala pa kazi.

Anakiri kuwa baadhi ya maofisa kwa serikalini walishafika kwenye mgodi huo na kutoa maelekezo na kwamba wanajipanga kurekebisha upungufu uliopo, ikiwamo kuwapima afya wafanyakazi, pamoja na kuanza kuwapatia vifaa kinga.

"Tunaomba radhi kwa usumbufu ambao umejitokeza kwa wafanyakazi wetu, upungufu wote tutaufanyia kazi na mtakuwa salama, pamoja na kutoa mikataba ya mwaka moja mmoja na kuonyesha pia kiwango cha mshahara, na utaandikwa kwa Kiingreza na Kiswahili, na mtasainishwa baada ya kumaliza kusoma," anaahidi Chao.

### SERIKALI YASHAURIWA

Rachel Changoja ni Mkurugenzi Mtendaji wa asasi ya HakiRasilimali, ikijishughulisha na masuala ya uziduaji katika sekta ya madini, mafuta na gesi, anasema kutokana na rasilimali hizo kumalizika na kutokana na kuchimbwa kuna haja ya serikali kuweka mkazo zaidi kisheria ili rasilimali zinufaishe Watanzania zaidi siyo kuwaachia ulemavu na mazingira yaliyoharibika.

Anakumbusha kuwa rasilimali hizo ni muhimu katika kubadilisha uchumi wa Watanzania, na kuweka historia kwa vizazi vijavyo kuwa katika nchi ilikuwa na madini na kuacha alama fulani kabla ya kumalizika.

"Kuna ulazima wa kutunga sheria mbalimbali za kuwabana wawekezaji ili kuwajali wazawa na kulipa kodi, kutunza mazingira na kupata uwekezaji wa kunufaika wahusika wote," anasema Changoja.



Uchimbaji madini hasa dhahabu ni kazi ngumu na hatari kwa wachimbaji kama sheria na taratibu hazitazingatiwa. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

**NA BEATRICE PHILEMON**



Wadau pamoja walimu na wanafunzi wa Shule ya Lusanga wakisikiliza mafanikio na matarajio ya mradi wa Eco-School Programme unaoendeshwa shuleni hapo. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

# Shule ilivyovuna maajabu baada ya kutunza misitu

WANAFUNZI na walimu wa Shule ya Msingi Lusanga iliyoko Mvomero, Mkoa wa Morogoro, wana kila sababu ya kufurahia, maana shule imejaa mafanikio, kuanzia ufaulu, ongezeko la mapato, mazingira bora ya kuishi na kusomea, lakini maisha ya majirani nao yamebadilika.

Hayo yanayokuja baada ya mradi wa Eco-School Programme kufanikisha ongezeko la ufaulu, kuboresha mazingira, shule kuanzisha vitalu vya miche ya miti mbao na matunda, bustani za mboga zinazouzwa kwa wateja mbalimbali ili kupata fedha kutatua changamoto zinazoikabili.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Lusanga, Ayoub Kihondo, anasema, anapozungumza na wanahabari na ofisa mradi wa Eco-School, kutoka Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) wanaotembelea shule hiyo hivi karibuni.

Lengo la ziara hiyo lilikuwa kuona mafanikio ya mradi kwa wanafunzi na jamii inayoizunguka shule kwenye kujiongezea kipato na kuinua elimu.

Kihondo anasema shule inajitegemea kimapato kutokana na fedha zinazokusanywa katika shughuli mbalimbali zinazofanywa na mradi wa Eco-Schools Programme, unatekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark kupitia Shirika la Danish Outdoor Council (DCC).

Anasema mradi huo, ulianza ra

> Mwaka 2017 wanafunzi 197 walifanya mtihani wa la saba , kati yao 129 walijiunga na sekondari, wavulana wakiwa 56 na wasichana 73.

**UCHUMI**

Akizungumzia eneo la uchumi, Mwalimu Kihondo, anasema shule imeuza miche ya miti mbao takribani 1,000 na kupata Sh. milioni 2.1 zilizotumika kukarabati darasa ambalo sasa ni ofisi ya walimu, kupiga rangi jengo la utawala, kukarabati ofisi na vyoo vya walimu.

"Tumeuza miche na mboga na kupata Sh. 3,000,000, tumetengeneza nguzo 50 kwa gharama ya Sh. milioni 1.5 na kuweka eneo la miche ya mbao, matunda na maua kila nguzo ikigharimu Sh.30,000 ," anasema Mwalimu Mkuu.

Aidha, anaongeza kuwa imenunua miche 200 ya mbegu za migomba zilizopandwa kwenye shamba la shule ili kupata chakula shuleni na kupunguza utoro, kujiongezea kipato na kuinua taaluma.

Anasema kati ya miche hiyo 200, mingine 100 ilitolewa kwa wanafunzi kupanda nyumbani ili kusambaza elimu ya kilimo cha migomba kwa jamii inayowazunguka.

Anasema fedha zinazopatikana kwa kuuza miche ya miti na migomba hutumiwa kuboresha miundombinu na kusafisha mazingira ya shule kama vile kununua sabuni za kunawa na kufanyia usafi.

"Kwa mwaka 2019 miche ya miti mbao na matunda zaidi ya 400 yenye thamani ya Sh. 200,000 ilitolewa bure kwa wanafunzi 558 wa darasa la saba, sita na tano ili wakapande nyumbani na mingine 14 walipewa wabunge wa mradi wa Eco-Schools....ili kueneza ujuzi wa kilimo cha miti kwa jamii inayotuzunguka na pia kujiongezea kipato." Anasema

Mwalimu Ayoub anawaomba watu kutembelea Shule ya Lusanga ili kununua miche ya miti, mboga na migomba ili kusaidia shule kupata fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo.

**TAALUMA**

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Lusanga, Ayoub Kihondo, anasema: "Hivi sasa kiwango cha taaluma ni kizuri kwa sababu ufaulu umeongezeka darasa la nne na la saba.

"Mwaka 2017 wanafunzi 197 walifanya mtihani wa la saba , kati yao 129 walijiunga na sekondari, wavulana wakiwa 56 na wasichana 73."

Mwaka 2018, waliofanya mtihani wa darasa la saba walikuwa 139 wanafunzi 120 walikwenda sekondari wasichana wakiwa 74 na wavulana 46. Wakati 2019, tulikuwa na wanafunzi 216 waliofanya mtihani wa la saba , 171 walichaguliwa kwenda sekondari wakiwa wasichana 99 na wavulana 72.

Anasema mwaka jana wanafunzi 75 walifanya mtihani huo na 71 walichaguliwa kujiunga na sekondari wasichana wakiwa 40 na wavulana 31.

**MAZINGIRA**

Mwalimu wa mazingira shule ya Lusanga, Omari Mohamed, anasema mradi Eco-Schools Programme umeboresha mazingira ya kujifunzia huku walimu wakiweka ujumbe wa mazingira kwenye masomo.

"Wanafunzi wanaelewa kuhusu utunzaji wa mazingira kwani tunatoa elimu kwa vitendo. Tunatumia muda mchache kufanya usafi tofauti na miaka ya nyuma kwa sababu wanafunzi wamepanda miti na nyasi katika eneo la shule ili kuzuia mmomonyoko wa udongo, kuna kivuli kwa ajili ya kujisomea, kulinda mazingira na bionuai." Mohamed anasema:

"Wanafunzi ni mabalozi wa kufikisha elimu kwa jamii kuhusu mazingira na wanafundisha wazazi jinsi ya kupanda miti na migomba kwani darasani tunafundisha kwa nadharia na shambani kwa matendo."

Anasema wanafunzi wakiwa nje ya darasa wanafundisha kwa vitendo kutunza miche ya miti, migomba na wamepanda wanafunzi wenyewe.

Anasema wanatoa watoto nje na kuwaonyesha mmea uliostawi na ambao haujastawi na ukamuuliza kwa nini huu umedumaa inakuwa rahisi kujibu wakieleza kuwa uliostawi, umemwagiliwa, una mbolea, kupaliliwa na unapata mwanga.

Anasema mradi umefanya wanafunzi wapende kujishughulisha au kufanya kazi kwa vitendo, kupenda mazingira na kuyatunza ili yaonekane bora na kuvutia.

Anasema watoto hufanya tathmini ya mazingira shuleni na kuunda darasa la mazingira na wameomba eneo la kupanda mihogo, viazi na mboga, mbolea na mbegu wanaleta wenyewe kutoka majumbani kwao na wanalenga kuvipanda shuleni.

Kupitia elimu waliyoipata, wanafunzi wanajiamini kuuliza maswali kuhusu masomo, tofauti na hapo awali, wanaomba vitabu kujisomea na mitihani ya miaka ya nyuma ili kuifanya na wanajiamini zaidi.

Mwanafunzi wa darasa la tano, Alex Atieni, Mbunge wa Kamati ya Eco-Schools shuleni hapo anasema, "tumefurahi mradi umetusaidia kujua vitu vingi kwenye mazingira, tumejifunza kupanda miti ya aina mbalimbali ya matunda, mbao na migomba... "Hivi sasa watoto wanatumia miti ya vivuli kujisomea na mzazi akijenga nyumba anafanya kama walivyofanya shule na pia kuwashauri wazazi kuanzisha bustani ya miti ya matunda na mbao na watoto wamekuwa walimu bora nyumbani kwao na wanafundisha wazazi kupanda migomba na miti," anasema.

Shule ya Msingi Lusanga iliyoanzishwa mwaka 1973 ina wanafunzi 1,162, walimu 13, madarasa tisa wakati inahitaji madarasa 13, kwani darasa la kwanza na la pili wanachangia darasa moja.





# Neema yaja kwa wakulima tumbaku

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania, imesema kuanzia Aprili mwaka huu, itaanza kutumia madaraja mapya ya zao hilo yatakayotumika kwenye masoko, ili kuwapa faida wakulima na kuwainua kiuchumi.

Madaraja hayo yamepungua kutoka 15 na kubaki matano.

Akizungumza katika kikao cha wataalamu na watendaji wa masoko ya tumbaku nchini, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo, Stanley Mnozya, alisema serikali imeamua kubadili madaraja ili kujibu kilio cha wakulima cha kulalamika kuwa hawapati faida kutokana na wingi wa madaraja ya awali.

Mnozya alisema madaraja ya zamani yalikuwa na adhabu nyingi kwa mkulima jambo lililosababisha kumnyima kipato.

Alifafanua awali kilo moja ya tumbaku ilikuwa inauzwa hadi Dola ya Marekani 0.5 kulingana na daraja la tumbaku, lakini kwa sasa inauzwa kuanzia Dola ya Marekani moja hadi mbili.

Mnozya alisema wamefanya mabadiliko ya madaraja ili kulinganisha na nchi jirani ambazo Tanzania inashindana nazo katika soko la tumbaku.

"Kwa sasa lugha ya madaraja ni moja na nchi ya Zambia, Malawi na Zimbabwe hii itasaidia nchi kujipima kuona wapi imefanya vizuri na wapi tunatakiwa turekebishe," alisema Mnozya.

Aidha, aliwasisitiza wakulima, wanunuzi, halmashauri na watendaji wote wa masoko kuwa zao la tumbaku linasifa nne kidunia ambazo lazima wapigane kuhakikisha zao hilo linafikia ili kujihakikishia soko la uhakika.

Alizitaja sifa hizo ni lazima tumbaku ilimwe ikiambatana na upandaji miti, kulima msimu unaofaa na vyama vihakikishe wakulima wanalipwa fedha zao baada ya mauzo.



Wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi kutoka Chama cha Wasioona Tanzania (TLB), Mkoa wa Dodoma, wakimsikiliza Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi, Ramadhani Mkude (hayupo pichani), wakati akitoa maelekezo kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wa viongozi, uliofanyika Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kero miundombinu mawasiliano yajadiliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imekutana na wadau mbalimbali wa mawasiliano kujadili namna ya kutatua kero ya miundombinu ya mawasiliano na kuilinda ili isihujumiwe, hivyo kuathiri uchumi.

Akifungua kikao hicho juzi, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisema tatizo la miundombinu ya mawasiliano kwa kiasi kikubwa zisipotatuliwa litaathiri uchumi wa nchi ambao wananchi ni watumiaji wakubwa. Alisema kwa sasa kuna kero nyingi ambazo zipo ikiwamo wizi wa mitandao, matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii.

"Hivyo tunaangalia namna ya kulinda miundombinu ili kuinua uchumi wetu na kuondokana na changamoto za wizi wa mitandao na matumizi mabaya yanayofanywa na watu," alisema.

Katibu huyo alisema kwa sasa wanataka kuhakikisha biashara mtandao, miamala ya kifedha iwe salama na ofisi zote zitumie mifumo iliyo salama.

Naye Mkurugenzi wa TEHAMA wa Wizara hiyo, Mulembwa Munaku, alikiri kuwapo kwa miundombinu ambayo ikihujumiwa inaathiri uchumi wa nchi.

"Tumekutana ili kuainisha vigezo vya miundombinu hii na kuweka utaratibu wa kuilinda na kuiendeleza ili kuondokana na hujuma ambazo huathiri mawasiliano," alisema.

Kwa upande wake, Mhadhiri kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Dk. Nkundwe Mwasaga, alisema kuna baadhi ya miundombinu ina umuhimu wake kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa nchi.

Aidha, alisema wanajadiliana kutengeneza regista ambayo itabeba mifumo.

Meneja Miundombinu ya Mawasiliano kutoka kampuni ya Vodacom kitengo cha Teknolojia, Michael Bujaga, alisema kikao hicho kinaenda kutafuta ufumbuzi katika mpango mkakati na uboreshaji miundombinu kwa ajili ya nchi nzima.

## Makandarasi barabara Bahi washauriwa ushirikishaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Donald Mejitii, amewataka makandarasi wanaojenga barabara wilayani humo kuwashirikisha wananchi kabla ya kuanza ujenzi ili kutambua njia za asili za kupita maji na kuondokana na uharibifu unaojitokeza mara kwa mara.

Mejetii aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika kikao maalum cha kujadili maendeleo na bajeti ya halmashauri hiyo.

Alisema baadhi ya barabara zimekuwa zikitengewa fedha na kutengenezwa, lakini msimu wa mvua unapofika barabara hizo huharibika na kutopitika.

"Naomba tusipeleke usomi bila kufanya utafiti, wananchi waishio eneo husika ndio wanajua historia ya maeneo, ukiwashirikisha watakueleza na utapata picha nzuri ambayo ukitengeneza barabara itadumu," alisema Mejetii.

Kadhalika, aliwataka madiwani kuongeza nguvu katika suala zima la ukusanyaji mapato na kudhibiti makazi holela.

Alisema kuna haja ya kuwa na mkakati katika ukusanyaji mapato kuanzia ngazi za vijiji.

"Suala la uanzishaji makazi holela lidhibitiwe kutokana na kuongezeka kwa vitongoji hali inayosababisha kuanzishwa shule shikizi kutokana na watoto kukaa mbali na shule."

"Zamani ilikuwa unakwenda shambani unalima unarudi sasa hivi wengi wanajenga mashambani na hivyo kuanzisha makazi holela ambayo yanahitaji shule, huduma za afya na maji, tuangalie namna ya kudhibiti uanzishaji makazi holela," alisema Mejetii.

Kwa upande wao, baadhi ya madiwani walitaka suala la upatikanaji wa maji kwa wananchi lipewe kipaumbele.

Diwani wa Kata ya Ibugule, Blandina Magawa, alisema katika vitongoji 13 hakuna vituo vya maji licha ya uhakiki kufanyika.

Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Charles Mduma, alisema bajeti ijayo imezingatia dira ya taifa ya maendeleo, ilani ya CCM na sheria ya bajeti.

Alisema wanaendelea na mpango wa utekelezaji wa ilani kwa miaka mitano kwa kutenga asilimia 40 ya mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo pia kutenga asilimia 10 kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na walemavu.



## Bil. 45.8/- kutumika Mbarali 2021/2022

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, limepitia na kupitisha mapendekezo ya rasimu ya bajeti kiasi cha Sh. bilioni 45.8 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato.

Akisoma taarifa hiyo kwenye Baraza la Madiwani, Ofisa Mipango wa Wilaya hiyo, Emmanuel Kishimba, alisema kati ya fedha hizo, mapato kutoka Serikali Kuu na wadau wa maendeleo ni Sh. bilioni 40 na mapato kutoka katika vyanzo vya ndani ni shilingi bilioni nne.

Alisema miongoni mwa vipaumbele katika rasimu hiyo ni kuhakikisha inafikia malengo ya kuwahudumia wananchi kupitia Mpango wa miaka mitatu 2021/22-2023/2024 kwenye sekta za kilimo, mifugo, elimu msingi, elimu sekondari, ardhi na maendeleo ya jamii.

"Rasimu ya bajeti kwa mwaka wa 2021/22 imejikita katika ujenzi miradi ya kimkakati ikiwamo Kituo cha Afya Utengule Usangu na Hospitali ya Wilaya, kuwezesha ukamilishaji wa ujenzi wa banio katika Skimu ya Umwagiliaji Ukwavila, kuwezesha ujenzi wa vivusha maji vitatu katika skimu ya umwagiliaji Msesule, kuwezesha usakafiaji wa mfereji mita 40 skimu ya umwagiliaji azimio," alisema Kishimba.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Tamimu Lubandamo, alisema moja ya vipaumbele ni kuhakikisha wanaendelea na ukamilishaji ujenzi wa vyumba vya madarasa, madawati na vituo vya afya.

Alisema katika kukamilisha masuala hayo watahamasisha nguvu kazi ya wananchi katika kuchangia pamoja na fedha kutoka serikalini.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya rasimu ya bajeti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali hadi kufikia Desemba, 2020, jumla ya Sh. bilioni 18.5 kutoka Serikali Kuu na fedha nyingine zilizopokelewa zilitokana na vyanzo vingine sawa na asilimia 40 ya fedha zote zilizoidhinishwa.

# Askofu ataka maombi ya corona

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

LICHA ya serikali kuendelea kuhamasisha wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi mapya ya virusi vya corona, Askofu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAMT), Zephania Mwalusambo, amesema dawa pekee ya kukabiliana na ugonjwa huo ni maombi.

Askofu Mwalusambo alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ibada na kwamba anaifananisha corona na ugonjwa wa tauni ambao ulizuka kipindi cha nyuma kama maandiko ya kwenye Biblia yanavyoeleza.

Alisema ugonjwa wa tauni uligharimu maisha ya wengi na kwamba dawa pekee iliyotumika kuumaliza ni maombi kwa Mungu.

"Kwenye Biblia tumesoma habari za mlipuko wa ugonjwa wa tauni, haukuwa na dawa, uliua watu wengi, lakini kitu pekee kilichosaidia kukabiliana na ugonjwa huo ni maombi, Wana wa Israel walimgeukia Mungu kuomba toba na kuwanusuru na ugonjwa, vivyo hivyo hata kwa corona tumtegemee yeye," alisema Askofu Mwalusambo.

Alitoa ushauri kwa dini zote kufanya mambo ya kufunga na kuomba ili kunusuru na janga hilo, na kwamba licha ya wataalamu wa afya kutoa maelekezo ya kujikinga na ugonjwa wa corona, lakini suluhisho ni maombi.

Alisema kanisa lake limekuwa likizingatia kanuni za usafi kwa kuhakikisha kabla na baada ya ibada kila muumini ananawa mikono kwa majisafi na sabuni na kwamba wanaendelea kukesha na kuomba Mungu kunusuru na janga la corona.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, alisema serikali imejipanga vyema kukabiliana na magonjwa mbalimbali yakiwamo yasiyoambukiza kwa kuwaanda wataalamu na vifaa tiba vya kisasa katika hospitali mbalimbali nchini.

Katika hatua nyingine, Askofu huyo, aliwashauri wanandoa kuendelea kudumisha upendo nyakati zote na kuachana na mazoea ya kuonyesha upendo kwa siku maalum kama vile Valentine.

Alisema upendo sio wa msimu na unatakiwa kuonyeshwa wakati wote na kwamba nyakati zimebadilika watu hawana upendo wa kweli kama wazee wa zamani badala yake wanaendekeza tamaa.

Hadi sasa serikali inaendelea kuwahamasisha wananchi kuendelea kuchukua tahadhari za magonjwa mbalimbali ikiwamo kuzingatia kanuni bora za afya.




Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mbeya, wakigombania usafiri wa daladala kurudi baada ya vipindi vya masomo kumalizika jana.
**PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Daladala walia bajaji kuvamia njia zao

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MADEREVA wa daladala katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wamemwomba Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kuingilia kati suala la uwapo wa bajaji, ambazo zinasafirisha abiria kwenye njia ambazo zimeainishwa kwa ajili ya daladala.

Wanadai kwamba changamoto hiyo inaathiri biashara yao, huku viongozi mkoani Mbeya wakishindwa kupata ufumbuzi.

Madereva hao waliyasema hayo juzi, wakati wakizungumza na Nipashe, ambapo walidai wamekuwa na kilio cha muda mrefu cha njia zao kuvamiwa na bajaj, lakini licha ya suala hilo kulifikisha kwenye mamlaka husika, hakuna hatua zinazochukuliwa ili kupata ufumbuzi wa kero hiyo.Mohamed Mshano, alisema hakuna hatua zozote zilizochukuliwa ili kuondoa kadhia hiyo ambayo imekuwa kero kwao kwani bajaji zinabeba abiria kwenye vituo vya daladala, suala ambalo ni kinyume cha makubaliano.

"Tulifikisha malalamiko yetu kwenye mamlaka mbalimbali ikiwamo Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) na Ofisi za Jiji, lakini hadi sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa ili kuondosha bajaji kwenye njia kuu au kuzipiga marufuku kupakia abiria kwenye vituo vya daladala, naamini kupitia vyombo vya habari serikali kuu itaweza kutusikiliza," alisema Mshano.

Akizungumzia malalamiko hayo, Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Mbeya, Denis Daud, alisema utaratibu wa kupanga ruti uko chini ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Alisema wanachokifanya ni kusimamia na kutekeleza kanuni na sheria za utumiaji wa vyombo vya moto na kuwaomba madereva hao kukaa meza moja na uongozi wa jiji ili kupata mwarobaini wa kero hiyo.Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema ni kosa kwa madereva bajaji kufanya ruti zinazofanywa na daladala na kwamba kwa mujibu wa maelekezo ni kwamba zinatumika kwa ajili ya kukodiwa tu.

Aliwaonya madereva bajaji wote kuacha tabia ya kufanya ruti za daladala wala kupakia abiria na kwamba watakaobainika kuvunja makubaliano hayo watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za usalama barabarani.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alikiri kukithiri kwa bajaji jijini Mbeya na kwamba kwa sasa hakuna sehemu ya kuzipeleka kwani vijana wengi wamepata ajira na wanaendesha maisha yao kupitia vyombo hivyo vya usafiri.

Alishauri madereva bajaji kuzingatia kanuni na sheria za usalama barabarani ikiwamo kuendesha kwa umakini na kuepusha msongamano kwenye barabara kuu ya Tanzania -Zambia (TANZAM)

Hata hivyo, madereva daladala wameiomba serikali kusimamia na kuzuia bajaji kutofanya ruti zinazofanywa na wao kwa madai kuwa wanapata hasara kwani abiria wengi wanakimbilia kwenye bajaji.





Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka, Issa Haji Gavu (kulia), akizungumza na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Ndoa kuvunjika chanzo udhalilishaji watoto'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhammed Said, amesema udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto kunatokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuvunjika kwa ndoa.

Alisema wizara anayoiongoza tangu mwaka 2016 ilifanya utafiti katika shule zote kuangalia chanzo cha udhalilishaji na kubaini matatizo ya ndoa husababisha watoto kukosa matunzo stahiki.

Akizungumza jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na kujibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa nafasi maalum, Saada Mkuya, aliyetaka kufahamu utafiti uliofanywa na wizara kujua chanzo cha udhalilishaji kwa watoto.

Mkuya alisema Zanzibar inakabiliwa na wimbi la udhalilishaji wa kijinsia, ikiwamo watoto, wanafunzi huku taarifa za vitendo hivyo zikionyesha hutokea kati ya walimu na wanafunzi au wananfunzi kwa wanafunzi wenyewe.

Waziri Simai alijibu kuwa kabla ya kufanywa kwa utafiti huo kumekuwa na ufuatiliaji na majadiliano ya kina kuhusu udhalilishaji wa watoto, hasa baada ya kutungwa kwa sheria ya kuwalinda wari na mtoto wa mzazi mmoja, Sheria Namba Nne ya Mwaka 2005.

Alisema matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa, chanzo cha udhalilishaji ni matumizi mabaya ya mitandao ya simu, tamaa, ukosefu wa malezi bora na kutofuatwa kanuni ya nidhamu za wanafunzi za mwaka 1996.

Alisema sababu zingine ni kutofuatwa kwa kanuni za miiko na maadili ya kazi za ualimu za mwaka 1995 na kutotumika ipasavyo kanuni ya adhabu ya viboko kwa wanafunzi ya mwaka 1988.

# SMZ: Uvuvi maeneo yaliyotengwa endelevu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu, imesema doria za uvuvi katika maeneo ya hifadhi yaliyotengwa na serikali ni endelevu kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu na rasilimali za baharini.

Hayo yalisemwa na Waziri wa wizara hiyo, Abdalla Hussein Kombo, wakati akitoa ufafanuzi na kujibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu, Haji Omar Kheir, aliyetaka kujua kwa nini wavuvi wanasumbuliwa wakati wanapofanya shughuli za uvuvi katika kisiwa cha Tumbatu.

Kombo alisema si kweli wavuvi wanasumbuliwa wakati wakifanya shughuli za uvuvi cha msingi wafuate sheria za uvuvi zilizopo.

Alieleza imebainika wapo wavuvi wanaendesha uvuvi katika maeneo ya hifadhi tengefu, ambayo yametengwa kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu.

Alisema kisiwa cha Tumbatu ni moja ya eneo tengefu lililopo katika hifadhi ya kitaifa na kuona rasilimali za uvuvi wa baharini zinalindwa.

"Mheshimiwa Spika, wapo wavuvi wanajipenyeza na kuendesha uvuvi haramu katika maeneo ya hifadhi ambayo yametengwa kwa ajili ya kulinda rasilimali za baharini," alisema Kombo.

Aliwataka wavuvi kuhakikisha wanafuata taratibu na sheria mbalimbali za kulinda rasilimali ya uvuvi wa baharini na kuacha kutumia mitego ambayo imepigwa marufuku na idara ya maendeleo ya uvuvi.

"Ipo sheria 11 ya Uvuvi ya Mwaka 2015 imepiga marufuku aina ya uvuvi ikiwamo wa kutumia mishale ambao unatishia uharibifu wa mazingira ya matumbawe ambayo ndiyo mazalia ya samaki na viumbe vya baharini," alisema.

# Katibu Mkuu Kiongozi atetea wanawake kwenye uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Zena Ahmed Said, ameitaka jamii kuachana na utamaduni potofu kwamba mwanamke akipewa nafasi, ni upendeleo ama zawadi.

Alisema baadhi ya jamii wana fikra mbovu kuwa mwanamke anapoteuliwa nafasi ya juu ya uongozi, ana uhusiano na mteuaji.

Aliyasema hayo juzi, akichangia katika mada kuhusu nafasi ya uongozi kwa wanawake wakati wa uzinduzi wa kitabu cha mwongozo wa ushiriki wao kwenye uongozi na siasa kilichotayarishwa na asasi za kiraia ikiwamo Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA)) mjini Zanzibar.

Alisema ni vyema kuondokana na fikra hizo kwa sababu wanawake wana uwezo na wanachaguliwa kwa vigezo.

Katibu Mkuu huyo aliwataka watendaji waliopo katika sehemu za maamuzi kutenda haki pale wanapokuwa na fursa za kuteua nafasi za uongozi bila ya kumnyima fursa mwanamke.

Alisema kuwa baadhi ya watu wamekuwa na mitazamo hasi dhidi ya mwanamke katika suala la kubeba mimba, wakidhani atashindwa kufanya kazi na kusema hali ya ujauzito isiwe kigezo cha kunyimwa fursa. "Hizi mimba tusipozipata kizazi kitaendelea? Mwenyezi Mungu ametupa sisi hii miundombinu, kubeba mtoto tumboni miezi tisa sio mchezo, hivyo mimba isiwe sababu ya kumnyima fursa mwanamke," alisema Zena. Aliongeza ikitokea mwanamke na mwanaume kulingana katika vigezo ni vyema mwanamke akapewa fursa kwa sababu ni muda mrefu aliwekwa nyuma kutokana na mfumo uliokuwapo.

"Mimi sio muumini wa kumpa mwanamke fursa wakati hana uwezo, lazima awe na uwezo, lakini inapotokea nafasi inagombewa na mwanamke na mwanaume na vigezo vyao vinafungana ni bora kuamua nafasi hiyo kuwapa wanawake na wanapopewa nafasi wala hawahitaji kubebwa wanaziweza," alisema Zena. Pia aliwataka wanawake kusoma, kujua haki zao na kwamba kutokujua ni rahisi kuonewa na kwamba baadhi ya watu hutumia dini vibaya kumkandamiza mwanamke.

Hata hivyo aliwataka wanaume kuondokana na hofu kwamba wanawake wakipata nafasi za uongozi watawadharau.

"Niwaambie wanaume waliomo kwenye ndoa waondokane na hofu kuwa, wake zenu wakipata nafasi za uongozi watawadharau hizo ni hofu tu hazina maana yoyote."

Alisema yeye aliolewa baada ya kumaliza kidato cha sita, nafasi zote za uongozi alizipata akiwa ndani ya ndoa yake na Juni mwaka huu, atatimiza miaka 29 ya ndoa.

Mwakilishi wa nafasi maalum za Rais, Saada Mkuya, alisema mimba sio kigezo kwa mwanamke kushindwa kuwajibika katika utendaji wa kazi, kwa sababu yeye alipokuwa waziri wa fedha aliwasilisha bajeti ya serikali akiwa na mimba bila ya watu kujua ni mjamzito wa miezi nane.

"Mimba sio sababu ya sisi wanawake kutofanya kazi, tusiwe viongozi na ndio Mungu ametupa sisi kubeba mimba kwa kuwa tunaweza," alisema Mkuya.

Akifunga mjadala huo Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, aliwataka wanawake kuwa na umoja na ushirikiano ili kuwaunga mkono waliopewa nafasi mbalimbali za uongozi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0782253676*

## KUPOTEA KWA PASSPORT

**JUMA ISMAIL KALU** anatangaza kupotelewa na **HATI YA KUSAFIRIA (PASSPORT)** Iliyotolewa kwa namba **S0653/0019 TAE 339494** iliyotolewa na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji **06/05/2020** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu. **Taarifa ya polisi IRI/IRI/RB/793744/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**(W)YA IRINGA MJINI WILAYA YA IRINGA**

**SHAURI LA NDOA NA.7/2021**

**MDAI: ASHA JUMA SWETA-MAWELEWELE**

**MDAIWA:HOSEA LUWONEKO KIONE-SINGIDA**

KWAKUWA MDAI AMELETA MADAI YAKE YA KUACHANA NA MDAIWA KWAHIYO UNAHITAJIKA KUHUDHURIA BINAFSI KATIKA TAREHE 19/2/2021 SAA 2.30 ASUBUHI KWA SHAURI HILO NI LAZIMA KULETA MASHAHIDI WENU NA HATI ZOTE ZINAZOHUSU SHAURI HILO.
USIPOFIKA SHAURI LITASIKILIZWA UPANDE MMOJA.


**HATI HII IMETOLEWA LEO 15.2.2021**
HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI.

## KUPOTEA KWA CHETI




**JOYCE PAULIN MUNISHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2421/0007** kilichotolewa na baraza la mawaziri kupitia shule ya secondary **STAR** mwaka **2012,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi **Polisi taarifa DAR/MAG/RB/88048/2021**

## KUPOTEA KWA VYETI



**PETRO MASANJA** anatangaza kupotelewa kwa vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba **S0955-0157** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **ISAGEHE** mwaka **2012**, na cheti cha chuo cha **AUGUSTINE MUHEZA INSTITUTE OF HEALTH SCIENCE** course ya **CLINICAL MEDICINE** namba ya usajili **CMTS/ST.AMIHAS/15/74** mwaka **2015,** yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/URA/RB/19422/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**PETRO M. MAWE** anatangaza kupotelewa kwa cheti kifuatavyo,cheti cha **VETA MUHEZA TANGA** na **LEAVING CERTIFICATE** namba ya usajili **TAG/DSC/10/2013/283,** course ya **DRIVING** mwaka **2016**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/URA/RB/19422/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JULIUS KIHIO NTULWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 307 ACN – TOYOTA LANDCRUISER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa ya Polisi: KOR/RB/224/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**Mjini Morogoro**
**Usimamizi wa mirathi**
**45/2021**

Ombi la **MANENO MACHOZI** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **MGENI SAID MACHOZI**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **23/02/ 2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 15/02/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GABRIEL GERVAS NGOWI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 892 CNJ SUZUKI** CARRY. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. **CONTROL No. 9910818216371.**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mwenyekiti jopo la BBI afariki dunia

**Nairobi,** KENYA

SENETA wa Garissa nchini Kenya, Mohamed Yusuf Haji, amefariki dunia katika Hospitali ya Aga Khan, mjini Nairobi alikokuwa anapata matibabu, kwa mujibu wa familia.

Yusuf Haji alifariki dunia jana akiwa na umri wa miaka 80.

Haji pia alikuwa mwenyekiti wa Jopo kazi la Maridhiano nchini Kenya, maarufu BBI (Building Bridges Initiative).

**Haji alistaafu katika uongozi wa utawala wa mikoa, mwaka 1998.**

Kadhalika, alijiunga na utawala wa maeneo nchini Kenya mwaka 1960 kama mkuu wa wilaya na kupanda ngazi hadi kuwa miongoni mwa makamishna maarufu mikoani.

Haji alistaafu katika uongozi wa utawala wa mikoa, mwaka 1998.

Mwaka 2002, aliteuliwa kuwa mbunge na mwaka 2007, akachaguliwa kama mbunge wa eneo la Ijara kwa tiketi ya Chama cha Kenya African National Union (KANU).

Wakati wa kifo chake, alikuwa anahudumu muhula wa pili kama seneta wa Garissa.

Rais Uhuru Kenyatta na viongozi wengine, walituma salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu Yusuf Haji.

Rais Kenyatta pia alituma salamu hizo kwa familia na wakazi wa kaunti ya Garissa kwa kumpoteza seneta wao.

"Kifo cha Haji ni pigo kubwa kwa nchi hasa katika kipindi cha mabadiliko ya BBI ambapo mchango wake kama kiongozi utakosekana kwa kiwango kikubwa," alisema Rais Kenyatta.

Katika ujumbe wake, Rais Kenyatta amemwomboleza mwanasiasa huyo mkongwe ambaye hadi kifo chake alikuwa Mwenyekiti wa Jopo la Maridhiano (BBI), kiongozi wa kujitegemea na mzalendo. **BBC**

## Jeshi lazingira mitaa, intaneti yazimwa

**Nay Pyi Taw,** MYANMAR

MAGARI ya kivita yametanda katika mitaa ya miji kadhaa nchini Myanmar huku kukiwa na ishara kwamba wanajeshi wanaandaa msako dhidi ya wanaopinga mapinduzi yaliyofanywa Februari Mosi, mwaka huu.

Mtandao wa inteneti umezimwa nchi nzima ingawa kuna juhudi za kimataifa kupinga hatua hiyo.

Katika Jimbo la Kaskazini la Kachin, vikosi vya usalama vilifyatua risasi katika siku ya tisa ya maandamano ya kupinga mapinduzi.

Ofisa maalum wa Umoja wa Mataifa nchini humo, aliwashutumu wanajeshi kwa kutangaza vita dhidi ya raia wasio na hatia.

Tom Andrews, mwandishi maalum wa Umoja wa Mataifa (UN), kuhusu Myanmar inayojulikana pia kama Burma, alisema majenerali walikuwa wakionyesha dalili za kukata tamaa na kuwajibika.

Balozi mbalimbali za nchi za magharibi zimehimiza jeshi kuonyesha weledi wakati huu nchi hiyo ikiwa katika kipindi kigumu.

Nchini humo, mamia ya maelfu ya waandamanaji wanajikusanya katika miji kadhaa kupinga mapinduzi hayo.

Katika mji wa Myitkyina, katika Jimbo la Kachin, risasi zilisikika wakati vikosi vya usalama vikipambana na waandamanaji.

Haikufahamika ikiwa ni risasi za mpira au ama moto zilitumika kuwatawanya waandamanaji hao.

Waandishi wa tano ni miongoni mwa waliokamatwa.

Mapinduzi nchini Myanmar yaliondoa serikali ya raia iliyoongozwa na Aung San Suu Kyi baada ya chama chake National League for Democracy (NLD) kikishinda katika uchaguzi.

Picha za video zilionyesha watu wakipiga kelele na kugonga masufuria kuwaonya jirani zao kuhusu uvamizi wa jeshi majira ya usiku.

Suu Kyi, Khin Maung Zaw, watazuiliwa rumande hadi Februari 17. **BBC**



Askari akiwa ameshika silaha wakati waandamanaji wanaopinga mapinduzi wakikusanyika mbele ya Benki ya Uchumi ya Myanmar, eneo la Mandalay, jana. **PICHA: AP**

## Mlipuko mpya ebola watangazwa Guinea

**Conakkry,** GUINEA

WIZARA ya Afya nchini Guinea, imesema wagonjwa waliohudhuria mazishi waliugua, kutapika na kutokwa na damu katika wilaya ndogo ya Goueke na wengine kutengwa katika vituo vya matibabu.

Kesi saba zilithibitishwa Kusini mwa nchi, ikiwa ni pamoja na vifo vinne.

Guinea ilitangaza mlipuko mpya wa ebola juzi, baada ya vipimo vya watu watatu kufariki na wanne kumwa Kusini Mashariki mwa nchi hiyo.

Wizara ya Afya katika taarifa yake. ilithibitisha kwamba watu hao walikuwa na virusi vya ebola.

Juzi mamlaka nchini humo ilikutana katika kikao cha dharura jijini Conakry ili kutafakari kwa makini kuhusu mbinu za kukabiliana na mlipuko huo.

Mkutano huo ulifanyika mbele ya Waziri wa Afya, Mamlaka ya kitaifa ya Usalama wa Afya (ANSS), Taasisi ya kitaifa ya Afya ya Umma na pia washirika ambao ni Umoja wa Mataifa, Shirika la Afya Duniani (WHO), MSF, Alima, CDC, Shirika la Msalaba Mwekundu na wengine.

Mlipuko wa kwanza wa ugonjwa huo ambao ulikuwa mbaya zaidi duniani, ulitokea Guinea kati ya mwaka wa 2013 na 2016.

Kwa mujibu wa kanuni za kimataifa za afya, serikali ya Guinea imetangaza ebola kuwa ni janga.

Mtu aliyezikwa tarehe Februari, Mosi, alikuwa muuguzi katika kituo cha afya na alifariki baada ya kuhamishwa kwa ajili ya matibabu Nzerekore, mji ulio karibu na mpaka wa Liberia na Ivory Coast.

Mlipuko wa kwanza ulianzia Nzerekore, shughuli nyingi za biashara kwenye mipaka iliyo karibu zilikwamisha juhudi za kudhibiti virusi hivyo.

Wakati huo, virusi hivyo vya ebola viliathiri takriban watu 11,000 kesi nyingi ziliripotiwa nchini Guinea, Liberia na Sierra Leone. **RFI/VOA**

## 20 wafa kwenye maporomoko

**Nganjuk,** INDONESIA

WATU 20 hawajulikani walipo baada ya kutokea maporomoko ya ardhi yaliyosababishwa na mvua kubwa.

Tukio hilo lilitokea juzi jioni katika mkoa wa Nganjuk, Java Mashariki wa Indonesia, huku 14 wakijeruhiwa.

Raditya Jati, Mkuu wa Kituo cha Habari na Mawasiliano cha Wakala wa Kitaifa wa Usimamizi wa Maafa, alisema maporomoko ya ardhi katika kijiji cha Ngetos Mkoa wa Nganjuk, yalisababisha uharibifu mkubwa katika nyumba nane.

Aliripoti habari kwamba watu 20 wametoweka na 14 wamejeruhiwa katika maporomoko ya ardhi.

Jati alisema kuwa utafutaji na uokoaji wa waliopotea na juhudi za kuwaokoa wale ambao wameathiriwa vibaya na maafa, zinaendelea.

Wakati huo huo, Jati alikumbusha kuwa familia 294 zimeathiriwa vibaya na mafuriko katika mkoa wa Pasuruan katika Jimbo la Java Mashariki. **TRT**

# NYUMBA YA ANCELOTTI YAVAMIWA



**LIVERPOOL,** England

NYUMBA ya kocha, Carlo Ancelotti wa Everton ilivamiwa na majambazi usiku wa kuamkia Jumamosi na kuibwa kisanduku kilichokuwa na fedha ambazo kiasi chake hakijajulikana, katika eneo la Hall Road East, Crosby, Merseyside.

Kwa mujibu wa maofisa wa polisi, hakuna mtu yeyote katika makazi hayo aliyejeruhiwa baada ya mtoto wake wa kike aliyekuwa ndani kutoa taarifa.

Maofisa hao wa polisi sasa wanafanya uchunguzi na wameomba yeyote aliye na habari kuhusu watu hao waliokuwa wamevalia mavazi yaliyowafunika uso kuwapa taarifa.

Ancelotti ambaye ni raia wa Italia aliteuliwa kuwa kocha wa Everton Desemba, mwaka juzi na akatia saini mkataba wa miaka minne na nusu pale uwanjani Goodison Park.

Mkataba wa Ancelotti unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu wa 2023-24.

Ancelotti mwenye umri wa miaka 61, anajivunia kunyanyua jumla ya mataji 20 katika historia yake ya ukocha.

Miongoni mwa mataji hayo ni manne ya Ligi Kuu katika mataifa manne tofauti na mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Neville ataka kipa mpya United

**MANCHESTER,** England

GARY Neville amesema Manchester United inahitaji kumsajili golikipa mpya ikiwa wanalitaka taji la Ligi Kuu England.

United wamejiingiza katika kinyang'anyiro cha taji msimu huu, lakini wana uwezekano wa kulikosa wakati Manchester City inashika nafasi ya kwanza kwenye ligi hiyo.

David De Gea alikuwa kwenye uangalizi na makosa kadhaa katika sare ya 3-3 na Everton mwishoni mwa wiki iliyopita, na Neville anahisi United wanahitaji kuondoa changamoto kwa kuingia sokoni kutafuta kipa wa kiwango cha juu.

"Lazima tuanze kuuliza maswali juu ya David De Gea, kwa kile anachofanya," alisema Neville akinukuliwa na Daily Mail.

"Anafanya makosa mara kwa mara na zaidi yanaigharimu timu."

Neville ameshawishika kusema kuwa kocha wa Manchester City, Pep Guardiola au bosi wa Liverpool, Jurgen Klopp, wangeweza kutatua shida haraka kama wangekuwa na nafasi hiyo pale Old Trafford, kwani anahisi pia msaidizi wa De Gea Dean Henderson sio suluhu ya tatizo.

"Kama Pep Guardiola au Klopp wangeingia Manchester United katika kipindi cha miezi sita, wangeleta kipa mpya," amesema Neville.






# *Conte awasifia Lukaku, Eriksen*

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku amejibu shutuma za hivi karibuni kwa kufunga dhidi ya Lazio na Christian Eriksen anaanza kuelewa kwanini Inter inamhitaji, amesema kocha wa Nerazzurri hao, Antonio Conte.

Inter ilitolewa kwenye mashindano ya Coppa Italia hatua ya nusu fainali baada ya kutoka sare ya bila kufungana na Juventus na kuiwezesha kusonga mbele kwa uwiano wa mabao 2-1, lakini ushindi wa 3-1 dhidi ya Lazio Jumapili ulishuhudia kikosi cha Conte kikiwapiku wapinzani wao AC Milan kileleni mwa msimamo wa Serie A.

Lukaku alifunga mara mbili kipindi cha kwanza na kufikisha mabao 300 aliyofunga kwa kipindi chake cha uchezaji, na Lautaro Martinez akafunga baada ya Gonzalo Escalante kuifungia Lazio pale katika dimba la San Siro.

Akizungumza kuhusu straika huyo wa kimataifa wa ubelgiji, Conte aliiambia Sky Sport: "Romelu, ni kama timu nzima, alitoa mchango mkubwa. Lautaro alifanya hivyo, kama Ivan Perisic, na mlinzi Marcelo Brozovic.

"Baadhi ya watu walianza kuzungumza kuhusu Lukaku baada ya kutolewa kwenye Coppa Italia, lakini kuna wakati mchezaji hawezi kuwa fiti kwa asilimia 100.

"Amerudi na kufunga na tunamhitaji Romelu wa hivi. Tunahitaji ubora wake na namna anavyoweza kuisaidia timu."

Eriksen alisajiliwa kutoka Tottenham Januari, 2020, lakini alikuwa kwenye wakati mgumu kupata nafasi ya kucheza.

Hata hivyo, mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark ameendeleza kiwango chake na kuwa mtulivu na sasa Conte anamsifia.

"Nafikiri Christian alikuwa na matatizo madogo ya kulielewa soka la Italia, ambalo ni gumu sana kwenye mbinu ukilinganisha na Ligi Kuu England.

"Lakini sasa anaonekana kuelewa na kwenda na kasi yetu," alisema Conte.

HABARI MICHEZO

# Chelsea njia nyeupe kwa Alaba

**LONDON,** England

MATUMAINI ya Chelsea ya kumsajili beki wa Bayern Munich, David Alaba yametiwa nguvu zaidi baada ya klabu hiyo ya Ujerumani kuthibitisha imemalizana na mlinzi, Dayot Upamecano kutoka RB Leipzig.


Kikosi cha Thomas Tuchel kilikuwa na matumaini yao ya kuimarisha ulinzi wao kwa kumsajili raia huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, na hivyo baada ya Bayern Munich kubainisha kuhusu Upamecano sasa ni wazi wana nafasi kubwa.

Alipoulizwa na gazeti la Bild ikiwa angeweza kuthibitisha kuwa makubaliano yamekubaliwa, Mkurugenzi wa Michezo wa Bayern, Hasan Salihamidzic alijibu: "Ninaweza, na tunafurahi sana kwa hilo hapa FC Bayern".

Wakiwa na uhakika wa kumsajili Upamecano, inaripotiwa kwamba hii inaweza kufaidisha nafasi ya Chelsea kumsajili Alaba katika kipindi cha msimu ujao wa joto.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Austria anatarajiwa kuwa mchezaji huru ifikapo Juni, mwaka huu, wakati mkataba wake na mabingwa hao wa Bundesliga utakapomalizika, na Blues ni moja ya klabu zinazoongoza katika mbio za kuwania saini yake.

Alaba ameichezea Bayern Munich zaidi ya mechi 400 tangu ajiunge na klabu hiyo mwaka 2009, ameshinda mataji tisa ya Bundesliga na mataji mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.





# KOCHA RB ALIKARIBIA CHELSEA

**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa RB Leipzig, Ralf Rangnick, amedai Chelsea walitaka kumwajiri kama mwalimu mpya wa muda kabla ya kumgeukia, Thomas Tuchel.

Frank Lampard aliondolewa majukumu yake pale Stamford Bridge Januari 25, mwaka huu na Tuchel aliletwa kama mbadala wake baada ya kukosa timu tangu alipotimuliwa na Paris Saint-Germain.

Rangnick pia alitajwa kuwa mshindani wa nafasi hiyo na sasa amethibitisha kuwa The Blues walimpa nafasi ya kuingia kwenye dimba hilo kwa muda.

Rangnick aliliambia gazeti la The Times juu ya mazungumzo yake na Chelsea: "Niliwaambia, ningependa kuja kufanya kazi pale, lakini siwezi kufanya hivyo kwa miezi minne. Mimi sio kocha wa muda."

Alipoulizwa ikiwa angekuwa wazi kuchukua nafasi tofauti katika Ligi Kuu England hapo baadaye, aliongeza: "Inapaswa kuwa kitu maalum. Inategemea klabu na ikiwa unataka kufanya kazi na kocha wa Ujerumani."

Mbali na Leipzig aliyoinoa kati ya mwaka 2015 na 2019, Rangnick amefundisha klabu 10 tofauti za nchini Ujerumani.

Schalke, Hoffenheim, Hannover na Stuttgart ni miongoni mwa timu alizofundisha kocha huyo mwenye umri wa miaka 62.

# *Guardiola: Ederson ni kipa bora*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amemtaja golikipa, Ederson kuwa ni namba moja bora zaidi.

Pasi ndefu kutoka kwa Ederson ilianzisha safari ya goli la Ilkay Gundogan katika ushindi wa mabao 3-0 wa Ligi Kuu England dhidi ya Tottenham, Jumamosi.

Guardiola hapo awali alidokeza kipa huyo anaweza kuwa mpigaji wa penalti wa City kutokana na uwezo wa miguu yake.

Baada ya kufanya kazi na Manuel Neuer huko Bayern Munich na Victor Valdes kule Barcelona, Guardiola alisema Ederson ndiye amekuwa bora zaidi kwa kutoa pasi.

"Kwa miguu yake, ndiye bora. Ubora wa kutoa pasi, ningesema, ndio bora zaidi."

"Manuel na Victor walikuwa wazuri sana pia, lakini kwa ubora wa pasi yeye ni bora zaidi. Sitasema ni nani aliye bora kwa jumla, kwa sababu nilikuwa na mafanikio hapo zamani na makipa, Victor, Manuel na Eddie.

City iko alama saba juu ya msimamo wa Ligi Kuu England, huku Jumatano ikiwa ugenini kucheza na Everton.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG SIRI ARSENAL KUNG'ARA

Kauli hiyo imetolewa na Arteta na kuongeza straika huyo amerejea katika ubora wake...

**LONDON,** England

KOCHA Mikel Arteta amezungumzia umuhimu wa Pierre-Emerick Aubameyang kwa Arsenal, akisisitiza ubora wa straika huyo ndio unabeba majaliwa ya klabu hiyo.

Aubameyang alianza kwenye mchezo wake wa Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza tangu Januari 18, mwaka huu na kufunga 'hat-trick' yake ya kwanza kwenye mashindano hayo, na kufikisha mabao 200 tangu aanze kucheza soka Ulaya, wakati Arsenal ikiifunga Leeds United mabao 4-2, juzi Jumapili.

Akiwa ameanza kufunga dakika ya 13, Aubameyang aliongeza goli la pili na kumfanya kuwa mchezaji wa tisa kufunga mabao 200, tangu alipoanza kucheza soka Ulaya akiwa kule Ligue 1 mwaka 2009.

**Hector Bellerin alifunga bao la tatu kabla ya Aubameyang kukamilisha hat-trick dakika mbili baadaye, ingawa Pascal Struijk na Helder Costa waliipa mabao ya kufutia machozi Leeds.**

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa timu hiyo ya Arteta kufunga mabao manne ya kwenye Ligi Kuu England pale katika dimba la Emirates tangu Julai, mwaka jana, msimu uliopita.

Baada ya mchezo huo, Arteta akazungumzia umuhimu wa Aubameyang mwenye umri wa miaka 31 kwa kikosi hicho cha Arsenal.

"Nafikiri alikuwa bora sana leo (juzi), alikuwa akifanya mazoezi kwa nguvu sana kwa wiki iliyopita, hivyo alirudi kwenye ubora wake," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari. "Kwa uhakika alionyesha kwamba yupo vizuri, mwenye njaa ya mafanikio na alikuwa muhimu zaidi kwa timu, sio tu kwa mabao yake kwamba yalifanya vizuri kutupa ushindi kwa Leeds, lakini pia alionekana kujituma sana.

"Tunajua kwamba mafanikio ya Arsenal yanabebwa na Auba hasa akiwa kwenye ubora wake.

"Akiwa kwenye kiwango cha juu, ndio huifanya Arsenal kuwa bora na bora zaidi."

## ZISIKUPITE

### LLORIS ANUKIA PSG

KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, anataka kumsajili golikipa wa Tottenham Hotspur, Hugo Lloris. ***(Football Insider)***

### TOMAS KUTUA ARSENAL

ARSENAL inakaribia kumsajili straika wa Sporting Lisbon, Tiago Tomas mwenye umri wa miaka 18 kipindi cha majira ya joto. ***(Sun)***

### ARSENAL, EDOUARD SAFI

ARSENAL imeambiwa inaweza kumsajili straika wa Celtic, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 23, kwa pauni milioni 15. ***(Express)***

### LIVERPOOL, CITY VITANI

LIVERPOOL na Manchester City zinamfuatilia kiungo wa Borussia Monchengladbach, lorian Neuhaus, mwenye umri wa miaka 23. ***(Kicker)***

### CEBALLOS KUUZWA JUMLA

KIUNGO wa Hispania, Dani Ceballos ataigharimu Arsenal pauni milioni 22 kama wanataka kumnunua moja kwa moja kutoka Real Madrid kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### LUIZ MAMBO MAZURI

MLINZI wa Timu ya Taifa ya Brazil, David Luiz mwenye umri wa miaka 33, anatarajiwa kuongezwa mkataba mpya na Arsenal. ***(Independent)***

### CELTIC KUMSAJILI BRADY

KLABU ya Celtic imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Burnley na Timu ya Taifa ya Ireland, Robbie Brady ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Mirror)***

### SANTOS NJIA MOJA

KLABU ya Burnley inafikiria kumsajili golikipa wa Marekani anayeichezea Benfica, Carlos Joaquim dos Santos mwenye umri wa miaka 20. ***(Sun)***

### AARONS ATAKIWA BAYERN

BAYERN Munich ipo kwenye mchakato wa kumshawishi mlinzi wa kulia wa Norwich City, Max Aarons mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### STURRIDGE KUREJEA

NEWCASTLE imepewa ofa ya kumsajili fowadi wa zamani wa Liverpool na Chelsea, Daniel Sturridge. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 amekuwa hana timu tangu alipoondoka Trabzonspor. ***(90Min)***

### COSTA KURUDI KWAO

STRAIKA wa zamani wa Chelsea na Atletico Madrid, Diego Costa yupo kwenye mazungumzo ya kujiunga na klabu yake ya utotoni, Palmeiras. Costa mwenye umri wa miaka 32, alikatisha mkataba wake na Atletico Januari mwaka huu. ***(Sky Sports)***

## HABARI MICHEZO

# KUIPELELEZA AS VITA ILITUSAIDIA - BARBARA

**Na Adam Fungamwango**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, amesema ushindi ambao timu yao iliupata katika mechi ya kwanza ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), ulichangiwa na mbinu 'mbadala'.

**Barbara aliliambia gazeti hili mechi hiyo haikuwa rahisi na kuitaja moja ya mbinu iliyowapa ushindi ni 'kuwapeleleza' vyema wapinzani wao.**

Kiongozi huyo alisema kwa sasa wao kama Simba wamewekeza sana kwenye 'kuwasoma na kupeleleza' wapinzani wao na ndiyo kwa kiasi kikubwa kimewafanya wapate ushindi wa bao 1-0 na kukaa kileleni kwenye kundi lao.

"Mpaka kuna mwenyekiti mmoja wa zamani wa klabu yetu amenipigia simu na kunipongeza akisema Barbara hongereni, kupata ushindi Congo si jambo rahisi," alisema kiongozi huyo.

Alisema mazingira yalikuwa magumu na haikuwa kazi rahisi kupata ushindi kama si wao viongozi, benchi la ufundi na wachezaji kupambana kufanya kazi iliyotakiwa kufanyika katika mechi hiyo.

"Haikuwa rahisi, unajua hivi sasa nimewekeza sana kwenye mbinu ya kuwasoma na kuwapeleleza wapinzani. Kujua nguvu yao iko wapi na udhaifu wao ulipo, ili kujua unapambana nayo vipi kuziba mianya na nguvu yao na kutumia udhaifu wao ili kupata ushindi," alisema Barbara.

Hivi karibuni, Simba ilimwongeza Mzimbabwe Culvin Mavhunga kwenye benchi la ufundi ambaye ni mchambuzi wa masuala ya soka, aliyekuwa akiifanyia kazi hiyo katika kikosi cha FC Patinum na Chama cha Soka nchini Zimbabwe.

Mavhunga ni mtaalamu wa kujua na kuchambua viwango vya wachezaji wa timu pinzani, hivyo klabu ya Simba baada ya mechi kati ya timu hiyo dhidi ya FC Patinum, ilimchukua kwa kazi hiyo tu ya kupeleleza na kujua mfumo, mbinu, nguvu na udhaifu wa timu pinzani.

Simba imesharejea nchini na itashuka tena dimbani Februari 23, mwaka huu kuwakaribisha Al Ahly katika mechi ya pili ya hatua ya makundi itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.




Mwanamuziki Kalala Junior (kulia), akiimba pamoja na Papii Kocha katika onyesho la bendi ya Tukuyu Sound lililofanyika katika usiku wa Valetine kwenye Ukumbi wa Mawasiliano Park jijini Dar es Salaam juzi. Bendi hiyo inamilikiwa na wanamuziki hao wawili. **PICHA: SABATO KASIKA**

# DStv yaja na chaneli ya kiafrika

**Na Mwandishi Wetu**

BURUDANI ndani ya DStv inazidi kuongezeka baada ya kuanza kuonyesha chaneli maarufu ya maisha halisi ya kiafrika ijulikanayo kama 'Honey' iliyoanzwa kupasua mawimbi kuanzia jana.

Chaneli hii inayoonekana DStv 173 imesheheni burudani huku ukiweza kushuhudia maisha ya watu mashuhuri wa Kiafrika wakiwa kwenye uhalisia wake na kutengenezwa na waandaji wenye vipaji. Hapa utashuhudia mapishi, mahusiano, harusi pamoja na maudhui mengine kutoka pande zote za dunia.

Kulingana na uwepo wa wanadada mashuhuri kama Pearl Umeh (Nigeria), Patricia Kihoro, Foi Wambui (Kenya), Anele Mdoda, Mbali Nkosi na Anele Zondo (Africa Kusini), hakika chaneli hii itakuwa bora na yenye mvuto muda wote.

DStv imekuwa kitovu cha burudani kwa wapenzi na watazamaji wa televisheni na kila wakati imekuwa mstari wa mbele kuweka chaneli nyingi za kiafrika na hivyo kupanua wigo wa kazi za kiafrika kuonekana zaidi na hivyo kuchangia kikamilifu katika kuhakikisha kuwa maudhui ya kiafrika yanapata nafasi kubwa.

Chaneli ya Honey ina vipindi vingi na vya kuvutia ikiwamo Pastors' wives ambayo ndani na kipindi hiki utakutana na wanawake walioweza kuongoza familia kwa kupitia misingi ya dini, Love swap inayoonyesha changamoto za mahusiano ambapo wapenzi wanabadilishana wapenzi wao kwa kupitia chakula cha nyumbani cha usiku.

Kila kipindi kitakuwa kinaelezea maoni waliyonayo na mambo waliyojifunza kutoka kwa wapenzi waliokutana nao siku hiyo.

Pia kuna kipindi cha Making the menu na ndani ya kipindi hiki, wanakutana wanablogu wa chakula wawili na kutengeneza chakula kisha mtu maarufu atahitaji kuonja na baadae mmiliki wa mgahawa ataamua ni chakula gani akiongeze kwenye mpango wake wa chakula yaani Menu.

## Yanga Princess yaota ubingwa

**Na Saada Akida**

KOCHA wa vinara wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Edna Lema, amesema suala la timu hiyo kuibuka mabingwa wa msimu huu 'anamwachia Mungu' lakini anaendelea kukijenga kikosi chake ili kuwa imara zaidi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Edna alisema safari hii ligi ni ngumu hivyo anakipanga vyema kikosi chake kukabiliana na ushindani kwa sababu ana imani malengo yake yatatimia.

Edna alisema hawezi kuiweka Simba kuwa ndio mpinzani pekee katika kuwania taji hilo msimu huu kwa sababu timu zote zinazoshiriki ligi hiyo zimekuwa zinaonyesha ubora na hakuna mechi rahisi.

Alisema wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya mzunguko wa pili wa ligi ambao unatarajia kufanyika kuanzia Ijumaa kwenye viwanja mbalimbali hapa nchini.

Yanga Princess inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 31 baada ya kucheza mechi 11 na itaanza mzunguko wa pili ugenini dhidi ya Tanzanite Queens (Fountain Gate) kwenye Uwanja wa Foutain Gate Arena, jijini Dodoma.

## Ngorongoro, Ghana majaribuni AFCON U-20

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), inatarajia kuanza kampeni ya kuwania ubingwa wa Afrika (Afcon U-20) kwa kuwakabili yosso wenzao wa Ghana katika mchezo wa Kundi C utakaochezwa kwenye Uwanja wa Stade Municipal de Nouadhibou nchini Mauritania.

Fainali hizo zilianza kufanyika rasmi juzi kwa wenyeji kuambulia kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Cameroon.

Kocha Mkuu wa Ngorongoro Heroes, Jamhuri Kihwelo 'Julio' alisema maandalizi ya mechi hiyo yamekamilika na kikubwa zaidi amewaandaa vijana wake kupata ushindi ili kujiweka kwenye nafasi salama.

Julio alisema wanawafahamu wapinzani wao kwa kuwaangalia katika baadhi ya mechi walizocheza hivi karibuni.

"Tunashukuru tumepata video zao, japo nyingine ni fupi, lakini mchezo wa mpira kikubwa ni kujiandaa vizuri," alisema Julio.

Alisema kwa kuwa ni mara ya kwanza kushiriki michuano hii, lakini pamoja na hayo si kigezo cha kupoteza.

Michezo

Jumanne Februari 16, 2021

Nipashe



Aubameyang siri Arsenal kung'ara UKURASA 22

**KUJIFUA...**



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya kwanza ya Kundi C ya Fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa vijana (Afcon U-20), dhidi ya Ghana itakayochezwa leo nchini Mauritania. **PICHA: TFF**

# YANGA: KAGERA SUGAR HAWAPONI

## ●●● Maxime naye awakumbusha kikosi chake hakijaja kufanya utalii kwa...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amewataka wachezaji wake kusahau matokeo ya mechi iliyopita na badala yake kuwekeza akili na nguvu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, jijini Dar es Salaam.

**Timu zote mbili zitashuka dimbani kesho zikiwa na kumbukumbu ya kugawana pointi, tena wapinzani wao wakisawazisha dakika za lala salama, Kagera Sugar ikibanwa na Gwambina FC huku Mbeya City ya jijini Mbeya ikiwa nyumbani iliwasimamisha vinara hao.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaze alisema baada ya kurejea kutoka Mbeya wanajipanga kwa ajili ya mchezo huo na tayari amewaelekeza wachezaji wake kuondoa mawazo kuhusiana na mechi iliyopita na sasa wanatakiwa kupambana kuvuna pointi tatu za mchezo uliopo mbele yao.

Kaze alisema mzunguko wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara umekuwa mgumu zaidi, hivyo wachezaji wanatakiwa kuongeza umakini na kujitoa katika kila dakika ya mchezo ili kufikia malengo.

Mrundi huyo alisema kila mchezaji anajua majukumu yake akiwa ndani ya uwanja na anawaamini vijana wake watakamilisha mikakati waliyonayo ili kuona wanapata ushindi na hatimaye kuibuka mabingwa wa msimu huu wa 2020/21.

"Tunatakiwa kupambana na vile vile kuwa makini, kuongeza utulivu kwa kutumia nafasi tunazozitengeneza, hakuna mechi rahisi kwa sasa kila timu inahitaji kupata pointi, tunaangalia maandalizi yetu pamoja na nguvu kubwa kwenye kusaka ushindi ndani ya dakika 90," alisema Kaze.

Kuhusiana na nyota wao, Saidi Ntibanzokiza, alisema hatakuwa sehemu ya mpango wa mechi hiyo kwa sababu anaendelea na matibabu huku golikipa, Ramadhani Kabwili na mlinzi, Abdallah Shaibu 'Ninja' wamerejea kikosini baada ya afya zao kuimarika.

Kocha huyo alisema wanaendelea kufanyia kazi upungufu walionao ili kuendelea kujiimarisha kupata matokeo chanya na kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12, kutoka mikoa mbalimbali.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema kikosi chake kimeshawasili jijini na kiko kamili kwa mchezo huo wa hatua ya lala salama.

Alisema mechi zote zilizobakia katika mzunguko wa pili ni sawa na fainali kwa sababu kila timu inashuka dimbani ikiwa inataka kukamilisha malengo yake.

"Kila timu iko katika malengo yake, hakuna ambaye amesharidhika, bado hakuna mwenye uhakika wa kutwaa ubingwa au kubakia kwenye ligi hii msimu ujao, hii inamaanisha kila dakika 90 utakazokuwa dimbani zitaamua hatima yako, ni mechi za mchakamchaka," Maxime alisema.

## Biashara yazidi kuitisha Simba

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha Simba kikitarajia kuanza safari ya kuelekea Mwanza na baadaye Musoma mkoani Mara, Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, amesema licha ya Wekundu wa Msimbazi kuwa na kikosi bora, wamejipanga kuwashangaza kwa kubakiza pointi zote nyumbani.

Biashara United inatarajia kuwakaribisha mabingwa hao watetezi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Karume Mjini Musoma.

Baraza alisema Simba ni kati ya timu bora na ina wachezaji wazuri, lakini yeye na vijana wake wameandaa 'mpango maalumu' wa kuvuna pointi tatu katika mechi hiyo ambayo watakutana na vigogo hao wa Tanzania.

"Hatuna hofu na ubora wa Simba, tutaingia uwanjani kupambana hadi tone la mwisho, hatuwaogopi bali tuna waheshimu kwa sababu ni timu kubwa, tutapambana kuhakikisha msimu huu tunabakiza pointi nyumbani, maana kwa msimu yote hatujawahi kubakiza pointi tatu katika ardhi ya nyumbani," alisema Baraza.

## Poulsen apewa miaka mitatu

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limetangaza kuingia mkataba wa miaka mitatu na Kim Poulsen kwa ajili ya kuifundisha timu ya Taifa (Taifa Stars).

Poulsen, raia wa Denmark ambaye aliwahi kuifundisha Stars na timu za vijana, amesaini mkataba huo na kurithi mikoba iliyoachwa na Etienne Ndayiragije.

Mrundi huyo alifikia hatua hiyo ya kuvunja mkataba wa kuiongoza Stars Februari 11, mwaka huu na aliishukuru TFF kwa kumwania huku shirikisho likimtakia kila la kheri atakakokwenda.

Kim ambaye awali aliletwa nchini na aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Jan Poulsen, aliwahi kuifundisha Stars kati ya mwaka 2012 na 2013.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >